This is a reproduction of a library book that was digitized by Google as part of an ongoing effort to preserve the information in books and make it universally accessible.

Google™ books

https://books.google.com

CHAMA CHA MAPINDUZI

# SERA YA MALEZI YA TAIFA KWA WATOTO NA VIJANA TANZANIA

HQ
792
T34
C52
1987

DODOMA 1987

Digitized by Google

HOOVER INSTITUTION
STANFORD LIBRARIES

Digitized by Google

CHAMA CHA MAPINDUZI

# SERA YA MALEZI YA TAIFA KWA WATOTO NA VIJANA TANZANIA

DODOMA 1987

Digitized by Google

Digitized by Google

# YALIYOMO

**Ukurasa**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ..... 1
1.0 MAANA YA MALEZI ..... 1
2.0 MAMBO YANAYOATHIRI MALEZI BORA TANZANIA ..... 2
3.0 HALI YA MALEZI ILIVYO HIVI SASA TANZANIA ..... 3
4.0 MADHUMUNI YA SERA YA MALEZI YA TAIFA ..... 4

**SURA YA PILI: MALEZI YA WATOTO WA MIAKA 0—14** ..... 6
5.0 MALEZI YA WATOTO WACHANGA MIAKA 0—3 ..... 6
5.1 Matunzo ya Wazazi ..... 6
5.2 Matunzo ya Mama Mja Mzito ..... 6
5.3 Matunzo ya Mtoto Anapozaliwa ..... 7
5.4 Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga ..... 8
5.5 Maeneo ya Kuanzishwa Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga ..... 8
5.6 Wajibu wa Kuanzisha na Kuendesha Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga ..... 9
5.7 Wajibu wa Jamii kwa Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga ..... 9
5.8 Wajibu wa Wizara Inayohusika na Afya na Ustawi wa Jamii kwa Vituo vya Kutunzia watoto Wachanga ..... 9
5.9 Wajibu wa Wizara Inayohusika na Viwanda na Biashara kwa Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga ..... 10
5.10 Wajibu wa Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga ..... 10

6.0 MALEZI YA WATOTO WADOGO: MIAKA 4—6 ..... 10
6.1 Mambo ya Kufunzwa Mtoto ..... 10
6.2 Wanaohusika Kutoa Mafunzo ..... 11
6.3 Njia za Kufundishia ..... 11
6.4 Wajibu wa Wazazi kwa Mtoto ..... 12

Digitized by Google

| | | |
|---|---|---|
| 6.5 | Wajibu wa Majirani | 13 |
| 6.6 | Shule za Watoto Wadogo | 13 |
| 7.0 | MALEZI YA WATOTO WA UMRI WA MIAKA 7—14 | 17 |
| 7.1 | Wajibu wa Wazazi kwa Mtoto wa Miaka 7—14 | 17 |
| 7.2 | Wajibu wa Majirani na Jamii kwa Mtoto wa Miaka 7—14 | 18 |
| 7.3 | Elimu ya Msingi | 18 |
| 7.4 | Wajibu wa Walimu wa Shule za Msingi | 21 |
| 7.5 | Wajibu wa Wizara ya Elimu Kuhusu Malezi ya Watoto wa Umri wa Miaka 7—14 | 22 |
| 7.6 | Wajibu wa Jumuiya ya Wazazi | 23 |
| 7.7. | Wajibu wa Wizara Inayohusika na Viwanda na Biashara na Wizara Inayohusika na Utalii na Maliasili | 24 |
| 7.8 | Wajibu wa Taasisi Nyinginezo na Jumuiya Mbalimbali Kuhusu Malezi ya Watoto | 24 |
| 7.9 | Wajibu wa Viongozi wa Chama na Serikali | 25 |
| 7.10 | Wajibu wa Serikali za Miji na Vijiji | 25 |
| **SURA YA TATU:** | **MALEZI YA VIJANA: MIAKA 15—25** | 26 |
| 8.0 | HALI YA UJANA NA MAHITAJI YAKE | 26 |
| 9.0 | MALEZI YA VIJANA NYUMBANI, SHULENI, VYUONI, JKT NA JKU | 29 |
| 9.1 | Wajibu wa Wazazi, Walimu na Viongozi wa Makambi | 29 |
| 9.2 | Malezi ya Vijana Katika Shule za Sekondari | 32 |
| 9.3 | Malezi ya Vijana Katika Vyuo | 34 |
| 9.4 | Wajibu wa Wizara ya Elimu, Wizara Nyingine na Mashirika yenye Vyuo na Shule za Sekondari | 35 |
| 9.5 | Wajibu wa Wizara inayohusika na mambo ya Kazi na Utumishi | 36 |
| 9.6 | Wajibu wa Waajiri na JUWATA kuhusu Vijana wanapoajiriwa | 36 |
| 10.0 | MALEZI YA VIJANA MIJINI NA VIJIJINI | 37 |
| 10.1 | Mambo yanayoathiri Malezi ya Vijana Mijini | 37 |
| 10.2 | Mambo yanayoathiri Malezi ya Vijana Vijijini | 38 |
| 10.3 | Wajibu wa Serikali na Wizara mbalimbali kuhusu Malezi ya Vijana Mijini na Vijijini | 38 |

Digitized by Google

10.4 Wajibu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) .......... 41
11.0 WAJIBU WA UMOJA WA VIJANA KUHUSU MALEZI YA VIJANA .......... 41
12.0 ELIMU YA FAMILIA .......... 42
13.0 NDOA KWA VIJANA .......... 43

SURA YA NNE: FAMILIA, URITHI, WATOTO NJE YA NDOA NA WATOTO WASIO WA KAWAIDA .......... 45
14.0 WAJIBU WA FAMILIA KATIKA MALEZI .. 45
15.0 URITHI WA MALI YA FAMILIA .......... 46
16.0 MATATIZO YA WATOTO WALIOKO NJE YA NDOA .......... 47
17.0 MATATIZO YA WATOTO WASIO WA KAWAIDA .......... 49
18.0 MWISHO .......... 50

Digitized by Google

Digitized by Google

SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

1.0. Maana ya Malezi

2.0. Mambo Yanayoathiri Malezi Bora Tanzania

3.0. Hali ya Malezi ilivyo hivi sasa Tanzania

4.0. Madhumuni ya Sera ya Malezi ya Taifa

## 1.0 Maana ya Malezi

1.1. Neno malezi au tendo la kumlea mtoto lina maana pana sana na kwa binadamu huanzia wakati wa mimba, kuzaliwa, utoto, ujana hadi utu uzima.

1.2. Kumlea mtoto kuna maana ya kumtoa gizani kusiko na uhakika wala usalama na kumwongoza mwangani kwenye uzoefu wa wahenga, wazazi na jamii. Kumlea mtoto vile vile kuna maana ya kumpa mahitaji ya lazima, kama vile chakula, mavazi, malazi na matibabu na kumpatia mahitaji ya burdani kama vile michezo na vifaa vya kuchezea. Kulea kuna maana ya kumtunza mtoto, kumhifadhi na kumkinga dhidi ya madhara, magonjwa na maadui ili apate kukua akiwa na afya njema ya mwili na akili na aliyetengemaa kwa maono.

1.3. Malezi pia yana maana ya kumwingiza mtoto katika jamii kwa kumfundisha maadili, mila na desturi za jamii, kumjengea fadhila na mwenendo mwema unaokubalika na jamii; kumfundisha itikadi na mambo ya siasa anayopaswa kuyafahamu ili apate kuwa raia mwema anayeujua wajibu wake na haki zake katika jamii au taifa. Kumlea mtoto kuna maana ya kumwelimisha na kumzoeza hatua kwa hatua matumizi ya viungo na kumpatia stadi mbali mbali ili aweze kujitegemea, kujiendeleza na kuhudumia jamii yake.



Digitized by Google

1.4. Kumlea mtoto ni pamoja na kumpa maarifa na uzoefu wa maisha katika mazingira yake na jinsi ya kuyakabili; kumzoeza kuwa na mwenendo wa udadisi wa kuweza kupima mambo na kuweza kupambanua mema na mabaya. Kumrudi anapopotoka na kumhimiza awe mwadilifu; kujenga na kustawisha utu wake na kumfanya muungwana, mwema, mwaminifu, mtendaji hodari na mwenye nidhamu ya kujituma, hekima na busara.

1.5. Kwa kifupi malezi ni shughuli zote za kumtunza mtoto, kumfundisha au kumpa maelekezo yatakayomsaidia katika kukuza vyema mwili wake, akili yake, maono yake, vipaji vyake, utashi na uhodari wake ili atakapofikia utu uzima awe mtu mwenye manufaa kwake yeye mwenyewe na kwa taifa lake. Suala la malezi ni jukumu la wazazi, jamii na taifa zima.

## 2.0 Mambo Yanayoathiri Malezi Bora Tanzania

Mambo yafuatayo yanaathiri malezi bora ya watoto na vijana hivi sasa hapa Tanzania:

2.1. Mila na desturi za makabila mbali mbali ambazo bado zinafuatwa na ambazo baadhi zinapingana na aina ya malezi yanayofaa kwa mtoto wa jamii ya Tanzania ya kisasa inayojenga ujamaa na kujitegemea, umoja wa kitaifa na inayotaka kuleta maendeleo.

2.2. Kuwepo kwa ukoloni mamboleo na mabaki ya athari za ukoloni mkongwe ambayo huathiri baadhi ya watu na kuwafanya wadharau hata zile mila na desturi zetu za jadi, ambazo zinafaa, na badala yake wathamini na kuiga zile za mataifa yaliyotutawala. Kwa watu wa namna hii, malezi bora ya watoto wa Tanzania ya kisasa maana yake ni yale malezi bora yaliyoandaliwa kwa ajili ya ustawi wa jamii za mataifa ya nje.

2.3. Hali duni ya uchumi ya familia na ya taifa pia ni jambo linalodhoofisha malezi bora ya watoto nchini. Mapato duni ya familia na ya taifa, upungufu wa bidhaa na huduma, kupanda kwa bei za bidhaa na huduma hizo, ukosefu wa chakula na mahitaji mengine muhimu husababisha maradhi, unyonge na



Digitized by Google

kufanya maisha ya mtoto yasiwe ya uhakika tangu wakati wa mimba, kuzaliwa, kukua hadi utu uzima.

2.4. Jambo lingine linaloathiri malezi bora ni uzazi usiokuwa na mpangilio ndani na nje ya ndoa, jambo ambalo husababisha matatizo katika utunzaji wa watoto na maisha ya wazazi wenyewe.

2.5. Kutokuwepo kwa maandalizi maalum kwa ajili ya watoto wanapofikia hatua ya ujana ya kuwawezesha kukabiliana na matatizo yanayoambatana na mabadiliko makubwa ya mwili, akili na maono katika hatua hiyo ya ukuaji. Upungufu huu husababisha watoto wengi kuchanganyikiwa, kupotoka na kukosa msimamo wanapoingia kwenye hatua ya ujana.

2.6. Ukosefu wa elimu na teknolojia husababisha familia zilizo nyingi zisiweze kuacha desturi na mila zisizofaa, zisiweze kufuata kanuni za afya bora na zisiweze kuwa na stadi zilizo bora, siyo tu kwa kutunzia watoto lakini pia kwa kuzalishia mali ya kutosha na chakula bora na cha kutosha.

2.7. Ugomvi katika ndoa husababisha ukosefu wa amani na utulivu katika familia na hata kuvunjika kwa ndoa. Jambo hili husababisha watoto kutangatanga na kutokuwa na malezi yenye uhakika.

2.8. Baadhi ya watu wazima, wazazi, walimu na viongozi hawana tabia nzuri za kuweza kuwa mfano bora kwa watoto na vijana. Ni walevi, wavuta bangi, wezi, wabadhirifu, waongo, wazembe na hawajiheshimu mbele ya watoto na vijana.

## 3.0. Hali ya Malezi Ilivyo Hivi Sasa Tanzania

3.1. Kutokuwepo kwa mfumo mmoja wa taifa juu ya malezi kumesababisha malezi ya watoto na vijana yaachiwe wazazi binafsi na baadhi ya vyombo na taasisi. Kwa sababu hiyo kila familia, kabila, taasisi na vyombo kadhaa binafsi vinawalea watoto na vijana hao kulingana na vile aonavyo kila mmoja wao.



Digitized by Google

3.2. Matokeo ni kwamba kumekuwa na pengo katika malezi na hivyo mila na desturi za kabila, familia na za kigeni zimechukua nafasi kubwa na hakuna mshikamano katika malezi ya watoto na vijana.

3.3. Kukosekana kwa mshikamano katika malezi husababisha watoto, vijana na hata watu wazima nchini kutofautiana katika mtazamo wao kuhusu mambo ya msingi kwa taifa kama vile:

3.3.1. Heshima na adabu mbele ya watu wenye umri mkubwa kuliko wao.

3.3.2. Heshima kwa watu wenye madaraka na viongozi.

3.3.3. Imani katika Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, Uzalendo na kujitolea katika ujenzi wa taifa.

3.3.4. Kuthamini kazi, haki, usawa, ushirikiano, uwezo na mahitaji ya binadamu wengine.

3.3.5. Mtindo wa kuishi, kunena na kutenda; kula na kuvaa.

## 4.0. Madhumuni ya Sera ya Malezi ya Taifa

Sera ya Malezi ya Taifa ina madhumuni yafuatayo:

4.1. Kuwa na mfumo mmoja wa taifa wa kulea watoto na vijana ambao utaongozwa na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ili kuondoa tofauti zilizopo hivi sasa.

4.2. Kuwa na mfumo maalum wa kulea watoto na vijana, ambao unazingatia mahitaji ya kukua vyema miili, akili na maono yao kama watu binafsi lakini wanaowiana vyema na jamii tunayokusudia kuijenga.

4.3. Kuweka utaratibu ambao utafanya utekelezaji wa sera yenyewe uwahusishe kwa ukamilifu wazazi, Serikali, taasisi mbalimbali na jamii nzima, katika kubeba wajibu wa kutekeleza na kusimamia shughuli zote zihusuzo malezi ya watoto na vijana katika taifa.



Digitized by Google

4.4. Kufafanua wajibu wa wazazi, jamii, taasisi mbalimbali na vyombo vya Serikali vinavyohusika na malezi katika utekelezaji wa utaratibu wa taifa kuhusu suala zima la malezi bora kwa watoto na vijana.

4.5. Kufafanua mambo yanayohitajika katika malezi ya watoto na vijana wa taifa hili la Tanzania.

Digitized by Google

# MALEZI YA WATOTO WA MIAKA 0—14

5.0. Malezi ya Watoto Wachanga: Miaka 0—3

6.0. Malezi ya Watoto Wadogo: Miaka 4—6

7.0. Malezi ya Watoto wa Umri wa Miaka 7—14

## 5.0. Malezi ya Watoto Wachanga: Miaka 0—3

### 5.1. *Matunzo ya Wazazi*

Matunzo ya watoto wa umri huu lazima uanze na matunzo ya wazazi wenyewe. Kuhusu matunzo ya wazazi mambo ya kutilia maanani ni:

5.1.1. Uzazi wa majira. Ifahamike kuwa kama mama atapata mimba na kuzaa haraka haraka, afya yake na ya watoto atakaowazaa itadhurika. Suala la uzazi wa majira lilizingatiwa sana katika jamii zetu tangu zamani na ni la jadi yetu.

5.1.2. Kula chakula bora na cha kutosha, kunywa maji safi na salama, kuangalia usafi wa mazingira, wa mwili na mavazi, kuwa na burdani kama vile michezo pamoja na mazoezi ya viungo.

5.1.3. Kupata huduma za kinga na tiba.

5.1.4. Kuwa na maisha ya upendo na kudumisha hali ya utengemano ndani ya nyumba, ushirikiano mzuri na majirani na kuwa na bidii ya kazi.

### 5.2. *Matunzo ya Mama Mja Mzito*

Wakati wa uja uzito mama aendelee kupata matunzo na yawe mazuri zaidi kuliko kawaida ili awe na afya njema ya mwili, akili na aliyetengemaa vyema kwa maono. Matunzo mazuri ya mama mja mzito ni matunzo mazuri ya mtoto ambaye



Digitized by Google

hajazaliwa. Mambo yafuatayo ni muhimu kwa mama mja mzito:

5.2.1. Kula chakula bora cha kutosha hasa cha kujenga mwili na kutia nguvu ili kuzaa mtoto mwenye afya.

5.2.2. Kupata mafunzo kuhusu matunzo na malezi bora ya mtoto.

5.2.3. Kuhudhuria kliniki kwa ratiba atakayopangiwa na Wakunga.

5.2.4. Kupata sindano zote zitakazowakinga dhidi ya magonjwa yeye na mtoto atakayemzaa, kama atakavyoelekezwa na Wakunga.

5.2.5. Kama mama mja mzito ni mnywaji wa pombe au mvutaji wa sigara au tumbaku, inambidi aache kabisa kwa kipindi hiki.

5.2.6. Katika kipindi hiki mama mja mzito anahitaji hali ya utulivu na amani. Kwa hiyo mume wake na au wale wote wanaohusiana naye wasimpe maudhi na bugudha.

5.2.7. Kujiweka katika hali ya usafi wa mwili wake, nguo zake na mazingira yake. Asivae mavazi yanayobana.

**5.3. *Matunzo ya Mtoto Anapozaliwa***

5.3.1. Mtoto akisha zaliwa mama aendelee kupata matunzo ya kula chakula bora ili aweze kutoa maziwa mengi kwa ajili ya mtoto. Pia aangalie usafi wa mwili, mavazi, mazingira na kunywa maji safi na salama. Apate mapumziko ya kutosha.

5.3.2. Mama ampeleke mtoto kliniki kwa ratiba atakayopangiwa na Wakunga, afuate ushauri wote atakaopewa na ahakikishe kuwa mtoto anapata sindano za kinga za magonjwa yote kama atakavyoelekezwa.

5.3.3. Ahakikishe kuwa mtoto daima yuko katika hali ya usafi wa mwili na mavazi na analala mahali panapofaa.

5.3.4. Maziwa ya mama ni bora zaidi kuliko maziwa ya makopo. Kwa hiyo mama ahakikishe anamnyonyesha mtoto wake na siyo kumpa maziwa ya makopo kila wakati.



Digitized by Google

5.3.5. Mtoto aendelee kunyonya maziwa ya mama yake tu hadi atimiapo umri wa miezi minne. Baada ya kipindi hiki aanze kulishwa vyakula vya aina nyingine hasa vile vyenye protini ili visaidie ukuaji wake.

5.3.6. Ili mtoto akue vizuri na kwa afya njema, pamoja na kumpa vyakula vingine, mtoto lazima anyonye kwa muda mrefu maziwa ya mama; kati ya mwaka mmoja na nusu hadi miaka miwili.

5.3.7. Baada ya mtoto kuzaliwa wazazi wahakikishe anaandikishwa.

5.3.8. Wazazi (baba na mama) wawe na upendo kati yao na kwa mtoto. Wasigombane mbele ya watoto na wasivunje ndoa yao la sivyo itaathiri malezi na ukuaji wa watoto.

5.3.9. Wazazi wapate mafunzo ya elimu ya afya kwa familia yatolewayo na vyombo mbalimbali kama radio, vituo vya afya, zahanati, n.k. Wizara inayohusika na Afya iendelee kuhakikisha kuwa mafunzo hayo yanatolewa.

5.3.10. Wazazi waanze kujenga tabia ya mtoto kuhusu kwa mfano heshima, namna ya kula, lugha nadhifu n.k.

5.3.11. Mtoto afanyiwe uchunguzi wa afya yake mara kwa mara na apate matibabu kila anapoumwa.

5.4. *Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga*

Vituo vya kutunzia watoto wachanga ni muhimu sana kwa sababu zifuatazo:

5.4.1. Kuhakikisha kuwa watoto wachanga wote nchini wanapata matunzo bora.

5.4.2. Kumwezesha mama kupata muda wa kushiriki kwa ukamilifu katika ujenzi wa taifa na kufanya shughuli nyinginezo.

**5.5.** ***Maeneo ya Kuanzishwa Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga***

Vituo vya kutunzia watoto wachanga vianzishwe katika maeneo yafuatayo:



Digitized by Google

5.5.1. Katika vijiji.

5.5.2. Katika maeneo ya kazi kama vile karibu na viwanda, ofisi za Serikali na Mashirika ya Umma.

5.5.3. Kwenye maeneo ya makazi ya watu mijini.

**5.6. *Wajibu wa Kuanzisha na Kuendesha Vituo vya Kutunzia Watoto Wachanga***

Watakaohusika katika kuanzisha na kuendesha vituo vya kutunzia watoto wachanga ni:

5.6.1. Mashirika ya Umma.

5.6.2. Idara na Ofisi za Serikali.

5.6.3. Halmashauri za Miji na Serikali za Vijiji.

5.6.4. Jumuiya mbalimbali

5.6.5. Mashirika binafsi yatakayojitolea.

- Wote hao wataanzisha vituo hivyo kulingana na utaratibu utakaowekwa na Serikali (Wizara inayohusika na Afya na Ustawi wa Jamii).

**5.7. *Wajibu wa Jamii kwa Vituo vya Kutunzia Watoto***

Jamii ikione kituo cha kutunzia watoto wachanga kuwa ni chao. Wakisaidie, wakitumikie na washiriki kwa ukamilifu kwa hali na mali katika uendeshaji wake.

**5.8. *Wajibu wa Wizara Inayohusika na Afya na Ustawi wa Jamii kwa Vituo vya Watoto Wachanga***

5.8.1. Itatayarisha utaratibu wa matunzo yenyewe katika vituo hivyo ambao utatumika kwa nchi nzima.

5.8.2. Itaendesha mafunzo ya walezi watakaotunza watoto wachanga katika vituo hivyo. Walezi katika vituo vya kutunzia watoto wachanga lazima wawe watu walioandaliwa barabara na wawe wenye uwezo na moyo wa kutunza watoto.

Digitized by Google

**5.9. *Wajibu wa Wizara Inayohusika na Viwanda na Biashara kwa Vituo vya Watoto Wachanga***

5.9.1. Itahakikisha kuwa maziwa na vyakula mbalimbali vinapatikana.

5.9.2. Itahakikisha kuwa vifaa vya kuchezea watoto vinapatikana.

5.9.3. Idhibiti bei za maziwa na vyakula mbali mbali na mavazi ya watoto ili wazazi waweze kumudu kuvinunua.

**5.10. *Wajibu wa Vituo vya Kutunzia Watoto***

Pamoja na kutekeleza utaratibu utakaotengenezwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu matunzo ya watoto wachanga katika vituo, vituo hivi vya kutunzia watoto wachanga vitakuwa na wajibu ufuatao:

5.10.1. Kujenga tabia za watoto hatua kwa hatua kuhusu heshima, adabu, unadhifu wa lugha, usafi wa mwili na mavazi, kusema kweli, upendo na ushirikiano.

5.10.2. Kufanya maandalizi mazuri ya kuwapatia watoto chakula bora wanapokuwa vituoni humo.

5.10.3. Kuwawezesha watoto hatua kwa hatua kutambua mazingira yao kwa kujua majina ya vitu, watu, miti, wanyama, wadudu n.k. waliomo humo.

5.10.4. Kushauriana na wazazi kuhusu mahitaji na matatizo ya watoto.

**6.0. Malezi ya Watoto Wadogo: Miaka 4—6**

Katika kipindi hiki mtoto ni mtambuzi na mvumbuzi wa mambo mengi na ana uwezo mkubwa wa kujifunza mambo kwa kuiga, kwa vitendo, nyimbo na michezo. Katika kipindi hiki mtoto aanze kuongozwa na kujengwa kwa kiasi cha kutosha katika malezi ili kumwekea msingi ulio madhubuti.

**6.1. *Mambo ya Kufunzwa Mtoto***

Katika umri huu, hatua kwa hatua, mtoto aanze kufunzwa mambo yafuatayo:



Digitized by Google

6.1.1. **Heshima, adabu, utii, ushirikiano, upendo, kufanya kazi, unadhifu wa lugha na mavazi, kutunza mali, kusema ukweli na kujihadhari.**

6.1.2. **Kanuni za afya bora kama vile usafi wa mwili wake, mazingira na mavazi yake.**

6.1.3. **Uchoraji, michezo, muziki, na sanaa nyinginezo mbalimbali ili aweze kuendeleza vipaji vyake.**

6.1.4. **Kuendeleza uwezo wao wa kutambua mazingira yao.**

**6.2.** ***Wanaohusika Kutoa Mafunzo***

Wanaohusika katika kutoa mafunzo kwa mtoto wa umri huu kuhusu mambo yaliyotajwa hapo juu kwa kuzingatia umri na mahitaji yao ni:

6.2.1. Wazazi nyumbani

6.2.2. Majirani na jamii yote kwa jumla

6.2.3. Shule za watoto wadogo

**6.3.** ***Njia za Kufundishia***

Njia zifuatazo zitumike katika kutolea mafunzo kwa watoto·

6.3.1. Kuonyesha mfano wa ile mienendo tunayokusudia kuiendeleza kwa mtoto. Katika kipindi hiki mtoto ni mwepesi sana wa kuiga matendo yote ya watu wazima. Kwa hiyo wazazi, majirani na watu wazima wengine wote, mbele ya watoto au mtoto, lazima waonyeshe mfano wa matendo mazuri ya:

(1) Heshima, adabu, utii, upendo na ushirikiano
(2) Usafi wa mwili, mavazi na mazingira
(3) Unadhifu wa lugha na mavazi
(4) Bidii na uhodari wa kazi.

6.3.2. Njia nyingine ni ya michezo na sanaa. Mtoto katika umri huu hupenda sana kucheza michezo mbali mbali ambayo ni pamoja na kuchora chora, kuandika andika, kuunda vitu vyenye umbo



Digitized by Google

halisi kama vile gari, nyumba n.k. Hapa anaanza kutumia vipaji vyake na uwezo wa viungo vyake na milango ya fahamu. Mtoto lazima apate wakati wa kutosha wa kucheza na vifaa vya kutosha vya kuchezea ili kuanza kuendeleza akili yake na vipaji vyake. Acheze nyumbani na pia acheze nje kwenye vikundi na watoto wenzie ili awe mchangamfu na akuze moyo wa ushirikiano.

6.3.3. Njia nyingine ni kwa wazazi, majirani na jamii kwa ujumla kumuonya mtoto kila anapopotoka.

### 6.4. *Wajibu wa Wazazi kwa Mtoto*

6.4.1. Wazazi wote wawili waonyeshe upendo kwa mtoto wakati wote.

6.4.2. Wawe mfano bora wa nidhamu, tabia na maadili mema katika kauli, matendo na haiba zao.

6.4.3. Wahakikishe kuwa familia ina nyumba bora ya kuishi, chakula cha kutosha na kilicho bora, mapato ya kutosha kuweza kumudu mahitaji mengine kadhaa ya mtoto na familia kwa jumla.

6.4.4. Daima wawe ni familia iliyotulia na kutengemaa. Wasiwe wanagombana mbele ya watoto.

6.4.5. Wawe wanasahihisha mienendo na matendo yasiyofaa ya mtoto kwa kuonya, kuhimiza na kuelekeza kwa upole na kwa kuonyesha mfano.

6.4.6. Wawe wanaonyesha kupenda, kuvutiwa na kufuatilia kazi za mtoto ili kufahamu maendeleo yake.

6.4.7. Wawe wanapokea na kutekeleza ushauri na maelekezo ya waganga, kliniki na walimu wa shule ya watoto wadogo anakosoma mtoto.

6.4.8. Wawe wanasifu matendo mazuri na kazi nzuri ya mtoto na kumpa moyo.



Digitized by Google

6.4.9. **Wamshirikishe mtoto katika kuotesha na kutunza mimea na miti ya nyumbani na kutunza wanyama kama vile kuku, ng'ombe, mbuzi, sungura, mbwa n.k.**

6.4.10. Wahakikishe kuwa yafuatayo yanafanyika:

(1) Mtoto apate chakula bora na cha kutosha.

(2) Mwili wake, mavazi yake na mahali anapolala daima pawe safi.

(3) Apate vifaa vya kuchezea na wakati wa kutosha wa kucheza na kupumzika.

(4) Apate burdani ya kutosha na ambayo imeandaliwa na kuratibiwa vizuri, hasa siku za sikukuu na sherehe mbali mbali.

(5) Apate vifaa vya kufanyia mazoezi ya baadhi ya masomo na shughuli afanyazo shuleni.

(6) Apimwe mara kwa mara na atibiwe anapoumwa.

6.4.11. Washiriki kwa ukamilifu katika ustawishaji wa shule za watoto wadogo na vituo vya watoto wachanga.

6.4.12. Wawalee watoto katika mila na imani zinazokubalika.

### 6.5. *Wajibu wa Majirani*

6.5.1. Wawe mfano kwa watoto katika matendo, kauli, mavazi, upendo na ushirikiano.

6.5.2. Wazee na hata vijana wenye umri mkubwa wanapaswa kuonya, kuelekeza, na kuwasahihisha watoto wanapokosea.

6.5.3. Jamii iione shule ya watoto wadogo kama yao na kuisaidia ipasavyo katika ustawishaji wake.

6.5.4. Jamii iwaheshimu na kuwasaidia ipasavyo walimu wa shule za watoto wadogo na kuangalia maslahi yao ipasavyo.

### 6.6. *Shule za Watoto Wadogo*

Katika umri huu wa kati ya miaka 4 hadi 6 mtoto apelekwe kwenye shule ya watoto wadogo. Hapa ni mahali ambapo mtoto anaandaliwa kwa ajili ya ile safari ndefu ya kupata elimu



Digitized by Google

**ya shuleni ambako walimu wana wajibu wa kuchukua nafasi ya wazazi katika kulea watoto na vijana ili wawe wanamapinduzi walio tayari kujenga nchi ya Ujamaa na Kujitegemea.**

**6.6.1. *Umuhimu wa Shule za Watoto Wadogo***

**Umuhimu wa shule za watoto wadogo ni:**

(1) **Kumshirikisha mtoto na watoto wenzie wa rika moja, jambo ambalo husaidia kukuza moyo wa ushirikiano na kupendana na ambalo linakidhi silika ya mtoto ya kupenda kucheza na kufanya shughuli na wenzake katika kikundi. Humfanya awe mchangamfu.**

(2) **Kumpa mtoto elimu ya kumwandaa kuweza kumudu vyema elimu ya msingi.**

(3) **Kuhakikisha kuwa watoto wadogo wanapata matunzo bora.**

(4) **Kupanua na kuendeleza maarifa yao na kuwapa nafasi ya kucheza na kujifunza chini ya uongozi wa watu wazima wenye utaalam wa kulea na kufunza watoto.**

(5) **Kuwapa nafasi wazazi ya kushiriki katika shughuli mbali mbali.**

6.6.2. *Mafunzo Katika Shule za Watoto Wadogo*

Katika shule hizi mafunzo na shughuli zote za watoto zitaendeshwa katika misingi iliyofafanuliwa katika Elimu ya Kujitegemea ili watoto waanze mapema kukuza:

(1) Moyo wa udadisi

(2) Moyo wa kujiamini

(3) Moyo wa uzalendo yaani moyo wa kulipenda taifa, kuwa tayari kulitumikia na kulilinda.

(4) Bidii na uhodari wa kazi

(5) Moyo wa ushirikiano na kupendana

(6) Moyo wa kupenda kufanya kazi kwa pamoja kwa faida ya wote

(7) Kuendeleza vipaji mbali mbali

(8) Kuthamini utamaduni wa taifa

(9) Kuthamini na kutunza mali ya Umma, kuhifadhi na kutumia vizuri mazingira ya asili ya nchi.



Digitized by Google

(10) Kuthamini demokrasi

(11) Heshima kwa wakubwa

(12) Utii wa sheria na kanuni za jamii

(13) Ukarimu na kuthamini ubinadamu

(14) Kupenda umoja.

6.6.3. *Wajibu wa Kufungua na Kuendesha Shule za Watoto Wadogo*
Watakaohusika na uanzishaji na uendeshaji wa shule za mafunzo ya watoto wadogo ni:

(1) Mashirika ya Umma

(2) Halmashauri za Miji na Serikali za Vijiji

(3) Idara na Ofisi mbali mbali za Serikali

(4) Jumuiya mbali mbali

(5) Mashirika binafsi yatakayojitolea.

6.6.4. *Maeneo ya Kufungua Shule za Watoto Wadogo*
Kwa vile kazi mojawapo ya shule za watoto wadogo ni kuwaandaa watoto kuingia shule za msingi, ni vyema kila inapowezekana shule hizo zifunguliwe kwenye kila eneo lenye shule za msingi kwa sababu zifuatazo:

(1) Wanaweza kufuatana na watoto wa shule za msingi na kwa hiyo wasihitaji kupelekwa na wazazi wao.

(2) Wataanza kuzoea mazingira ya shule za msingi.

6.6.5. *Wajibu wa Wizara ya Elimu kwa Shule za Watoto Wadogo*
Wizara ya Elimu itakuwa na wajibu ufuatao kwa Shule za Watoto Wadogo:

(1) Itatayarisha mfumo wa mafunzo na shughuli za watoto katika shule za watoto wadogo ambao ni pamoja na mitaala, mihutasari na vitabu.

Digitized by Google

(2) Itatengeneza utaratibu wa Elimu ya Awali nchini.

(3) Itaendesha mafunzo ya walimu maalum wa kulea, kutunza na kufundisha watoto katika shule za watoto wadogo. Walimu wa kufundisha katika shule za watoto wadogo lazima waandaliwe barabara na wawe maalum kwa ajili hiyo.

(4) Itasajili shule hizo na kukagua shughuli zake.

6.6.6. *Wajibu wa Walimu wa Shule za Watoto Wadogo*

Walimu watachukua wajibu kamili wa wazazi kwa muda wote ambao watoto watakuwa mikononi mwao katika shule ya watoto wadogo. Kwa hiyo wana wajibu ufuatao:

(1) Kuwapenda watoto

(2) Zaidi ya kuwa na ujuzi wa kazi ya kulea na kutunza watoto pia wawe na moyo wa kuipenda na kuithamini kazi hiyo

(3) Wawe mfano halisi wa wao wenyewe kutimiza kwa kauli na vitendo mwenendo wa kuwa na heshima, adabu, upendo, ushirikiano, usafi wa mwili, mavazi na mazingira, unadhifu wa lugha, bidii na uhodari wa kazi.

(4) Wawe wanasahihisha matendo yasiyofaa ya watoto kwa kuonya na kuelekeza kwa upole na upendo.

(5) Wawe wanasifu matendo mazuri na kazi nzuri za watoto na kuzitangaza kama mfano kwa wengine.

(6) Wahakikishe kuwa watoto wanapata chakula bora na cha kutosha wanapokuwa shuleni. Katika jambo hili watashirikiana na wazazi na mamlaka inayohusika na uendeshaji wa shule hiyo.

(7) Wawe wanashauri na kuwaelekeza wazazi wa mtoto kuhusu mwenendo wa mtoto, afya yake, kazi na vipaji vyake vinavyopaswa kuendelezwa.

(8) Wahakikishe kuwa majengo na mazingira ya shule yanatunzwa vizuri na kuwekwa katika hali ya kuvutia.



Digitized by Google

## 7.0. Malezi ya Watoto wa Umri wa Miaka 7—14

Katika umri huu watoto wanapaswa kuwa katika shule za msingi. Kwa hiyo **shule za msingi na walimu wa shule** hizi wana nafasi kubwa ya kuwalea watoto wa umri huu katika misingi ya taifa na jamii kwa jumla. Hata hivyo msaada wa wazazi, majirani na jamii bado unahitajika.

### 7.1. *Wajibu wa Wazazi kwa Mtoto wa Miaka 7—14*

7.1.1. Waendelee kuwa mfano bora wa mwenendo wa heshima, adabu, upendo na ushirikiano, usafi wa mwili, mavazi na mazingira, unadhifu wa lugha, bidii na uhodari wa kazi.

7.1.2. Wahakikishe kuwa mtoto wao anarudi nyumbani moja kwa moja mara baada ya saa za masomo.

7.1.3. Baada ya mtoto kula na kupumzika wampe kazi za nyumbani za kusaidia wazazi hao kama vile kusafisha mazingira, kufua nguo, kuogesha wadogo zake, kazi za shambani au bustanini, kuchota maji, kutwanga au kwenda kusagisha nafaka, n.k.

7.1.4. Wazazi wawape watoto shughuli ndogo ndogo za uchumi ambazo zitakuwa mali ya watoto kama vile vishamba, bustani, n.k. ili watoto waanze kujitegemea.

7.1.5. Wawe na wakati wa kuzungumza na mtoto ili wajue matatizo aliyo nayo na pia kumpa hadithi, wasia na masimulizi yenye mafunzo ya maisha.

7.1.6. Kabla ya mtoto kwenda kulala wahakikishe anapata wakati wa kufanya kazi za masomo alizopewa na walimu kufanyia nyumbani au kufanya rejea ya mambo aliyojifunza siku hiyo.

7.1.7. Wasimamie kwa ukamilifu nidhamu ya mtoto kama inavyotakiwa na shule yake; kama vile kuwahimiza:

(1) Kuwahi shuleni

(2) Kuvaa sare ya shule

(3) Kuvaa mavazi ya heshima


Digitized by Google

**(4) Kutii sheria za shule, walimu na viongozi wa wanafunzi**
**(5) Kuheshimu walimu**
**(6) Kuwa na adabu kwa wakubwa na watoto wenzie.**

7.1.8. Wawafundishe mila na desturi zilizo nadhifu, imani, kanuni na sheria mbali mbali zinazotawala maisha ya kila siku.

7.1.9. Wawe wanapokea na kutekeleza ipasavyo ushauri na maelekezo ya walimu kuhusu mtoto wao.

7.1.10. Wawathamini na kuwaheshimu walimu wa shule za msingi na kuwapa kila msaada wanaohitaji ili wafanikishe shughuli zao.

7.1.11. Shule waione ni yao na washiriki kwa ukamilifu kwa hali na mali, katika shughuli za maendeleo na za ustawi wa shule hiyo na katika uongozi unaowahusu kama vile Kamati ya Shule n.k.

7.1.12. Washiriki katika vikao vya pamoja na walimu vya kujadili maendeleo na matatizo ya watoto na ya shule kwa jumla.

7.1.13. Wawe wanatembelea shule na walimu ili kudumisha uhusiano mzuri.

**7.2. *Wajibu wa Majirani na Jamii kwa Mtoto wa Miaka 7—14***

7.2.1. Wawe mfano bora wa heshima, adabu, utii, ushirikiano, upendo, bidii ya kazi, unadhifu wa lugha na mavazi, utunzaji wa mali na kusema ukweli.

7.2.2. Jamii iione shule ya msingi ni yao na washiriki kwa ukamilifu, kwa hali na mali, katika shughuli za maendeleo na ustawi wake.

7.2.3. Iwaheshimu na kuwathamini walimu na kuwapa kila msaada ili wafanikishe kazi zao.

7.2.4. Jamii iangalie maslahi ya walimu ipasavyo.

**7.3. *Elimu ya Msingi***

7.3.1. Elimu ya Msingi iwe kamili na yenye kujitosheleza kwa kuweza



Digitized by Google

kumpatia mtoto stadi na maarifa ili anapomaliza mafunzo aweze kujitegemea na kumudu maisha kwa ukamilifu popote anapoishi, iwe kijijini au mjini.

7.3.2. Iwe elimu inayompatia mtoto fikira, mwenendo na mtazamo utakaomfanya amalizapo mafunzo akubalike, awiane na aweze kuishi kijamaa, kuthamini umoja wa kitaifa, na kusaidia kuleta maendeleo.

7.3.3. Mafunzo ya nadharia yawe yanaoanishwa na vitendo.

7.3.4. Wanafunzi wawe wanafanya kazi za kuzalisha mali, chakula na vifaa kama sehemu ya mafunzo yao ili shule ijitegemee.

7.3.5. Kazi zote za uzalishaji mali shuleni ziendeshwe kitaalam ili ziwe mfano wa kuigwa na jamii inayoizunguka shule.

7.3.6. Wanafunzi wawe wanashiriki katika kazi za maendeleo katika jamii inayoizunguka shule kama sehemu ya malezi yao.

7.3.7. Mitihani, mazoezi na majaribio yawe yanapima mambo yote; taaluma iliyofundishwa darasani, mwenendo wa mtoto na makadirio ya kazi alizofanya kwa ajili ya shule yake, maendeleo ya jamii na taifa.

7.3.8. Mafunzo na shughuli zote za wanafunzi ziendeshwe katika misingi ya Ujamaa na ya Elimu ya Kujitegemea ili watoto waendeleze na kuimarisha:

(1) Moyo wa udadisi

(2) Moyo wa kujiamini

(3) Moyo wa uzalendo yaani kulipenda, kulitumikia na kulilinda taifa.

(4) Bidii na uhodari wa kazi

(5) Moyo wa ushirikiano na kupendana

(6) Moyo wa kupenda kufanya kazi kwa pamoja na kugawana mapato kwa usawa.

Digitized by Google

(7) Kuendeleza vipaji mbali mbali

(8) Kuthamini utamaduni wa taifa

(9) Kuthamini na kutunza mali ya umma, kuhifadhi na kutumia vizuri mazingira na maliasili ya nchi.

(10) Kuthamini demokrasi

(11) Heshima kwa wakubwa

(12) Utii wa sheria na kanuni za jamii

(13) Ukarimu na kuthamini ubinadamu

(14) Kupenda umoja.

7.3.9. Kila inapowezekana mwanafunzi, pamoja na kuzalisha bidhaa au kifaa ambacho kitakuwa mali ya shule, apewe fursa ya kuzalisha bidhaa fulani fulani au kifaa ambacho pia kitakuwa mali yake mwenyewe binafsi. Kwa mfano kama shule ina eneo kubwa la ardhi, wanafunzi wanaweza kuwa na bustani au vijishamba vyao binafsi n.k.

7.3.10. Njia za kufundishia ziwe:

(1) Njia za uvumbuzi

(2) Zinazowapa watoto shughuli na vitendo halisi.

(3) Zinazowapa watoto kazi za kufanya mmoja mmoja na katika vikundi

7.3.11. Masomo ya Sayansi yafundishwe kwa makini na wanafunzi wajifunze kufikiri na kutatua matatizo kisayansi na wajifunze teknolojia itakayowafaa katika maisha yao ya baadaye kama vile kutengeneza majiko ya kutumia kuni chache n.k.

7.3.12. Michezo, bendi na ukakamavu vitiliwe maanani shuleni na watoto wawe na fursa ya kufanya shughuli kwa ajili ya kupitisha wakati baada ya masomo kulingana na shauku zao.



Digitized by Google

7.3.13. Shule ziwe mahali pa kuwajenga watoto katika msingi madhubuti wa utii wa sheria na nidhamu. Kwa hiyo kila shule iwe na sheria na taratibu zilizopangwa vizuri na ihakikishe kuwa watoto wanazifuata kila wakati.

7.3.14. Kanuni za Afya ya Msingi zifundishwe kwa watoto shuleni na watakiwe kuzizingatia.

7.3.15. Elimu ya Siasa ifundishwe kwa ukamilifu ili watoto waijue siasa na mfumo unaotawala nchi yao. Wafundishwe sheria zinazohusu maisha yao ya kila siku ili wajue haki zao na wajibu wao kama raia.

7.3.16. Kuwepo na vyama na vikundi mbali mbali ambavyo watoto wataweza kujiunga, kama vile Chipukizi, Skauti wa kiume na kike, kwaya na vikundi vya sanaa mbali mbali.

### 7.4. *Wajibu wa Walimu wa Shule za Msingi*

7.4.1. Watoto wanapokuwa shuleni, walimu wanachukua nafasi kamili ya wazazi wao. Kwa hiyo walimu wawapende watoto na wawe mfano bora wa heshima, adabu, upendo na ushirikiano, usafi wa mwili, mavazi na mazingira, unadhifu wa lugha, bidii na uhodari wa kazi.

7.4.2. Wawe wavumilivu na wasikivu kwa matendo, matatizo na hulka za watoto. Waangalie afya zao na wahakikishe wanapata tiba kila inapobidi.

7.4.3. Watekeleze na kusimamia kwa ukamilifu mambo yote yaliyofafanuliwa kuhusu Elimu ya Msingi katika Sera hii ya malezi.

7.4.4. Wafuatilie kwa makini kazi, tabia, shauku na vipaji vya kila mwanafunzi ili waweze kumsaidia, kumrekebisha na kumwendeleza.

7.4.5. Wawe wanasifu matendo mazuri na kazi nzuri za watoto na kuwapa moyo.



Digitized by Google

7.4.6. Watunze kumbukumbu kuhusu maendeleo na mwenendo wa kila mwanafunzi.

7.4.7. Watoe taarifa za mara kwa mara kwa wazazi au walezi kuhusu kazi, tabia, shauku na vipaji vya mwanafunzi na kuwashauri ipasavyo ili wazazi nao wasaidie katika kuwarekebisha au kuwaendeleza.

7.4.8. Wadumishe uhusiano mzuri kati yao na wazazi na wawashirikishe katika shughuli za maendeleo, ustawi, uongozi na utatuzi wa matatizo ya shule na ya wanafunzi. Wawe wanawatembelea wazazi nyumbani ili kudumisha uhusiano mzuri.

7.4.9. Wawe mfano wa tabia nzuri katika jamii na washiriki kwa ukamilifu katika shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii. Daima wawe tayari kutoa ujuzi, ushauri na utaalam wao kwa manufaa ya jamii kila unapohitajika.

7.4.10. Wakishirikiana na wazazi, wahakikishe kuwa watoto wanapokuwa shuleni wanapata chakula cha kutosha na kilicho bora.

7.4.11. Wawashirikishe wanafunzi katika uongozi wa shule na katika uamuzi wa baadhi ya mambo ambayo yanawahusu.

7.4.12. Walimu wawe ni watu wenye kupenda kujisomea na kujiendeleza kila wakati katika elimu, ili kuongeza ujuzi na maarifa yao na mbinu zao za kufundishia na kulelea watoto.

7.4.13. Wahakikishe kuwa vifaa, majengo na mazingira ya shule yanatunzwa ipasavyo na kuwekwa katika hali ya kuvutia.

**7.5. *Wajibu wa Wizara ya Elimu Kuhusu Malezi ya Watoto wa Umri wa Miaka 7—14***

7.5.1. Isimamie kwa ukamilifu utekelezaji wa sehemu za Sera hii ya Malezi ya Taifa zinazohusu Wizara yenyewe, Shule, Walimu na Wanafunzi.



Digitized by Google

7.5.2. Wizara ya Elimu iendelee kuandaa mitaala na mihutasari ya masomo ambayo ni ya aina moja kwa nchi nzima na ambayo inazingatia mtazamo wa taifa kuhusu malezi ya watoto kama ulivyofafanuliwa katika Sera hii ya Malezi.

7.5.3. Itaendesha mafunzo ya walimu kwa ajili ya shule za msingi.

7.5.4. Iweke sheria na taratibu za kuwabana wazazi watimize wajibu wao kwa watoto wao shuleni.

7.5.5. Ikishirikiana na Serikali za Mitaa ihakikishe kuwa Shule za Msingi zina walimu, vifaa na vitabu vya kutosha.

7.5.6. Ikague shule zote mara kwa mara ili ifahamu matatizo yake na utatuzi wake na kuzisaidia ziweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi.

7.5.7. Isimamie kwa ukamilifu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Kujitegmea katika shule zote.

7.5.8. Iangalie maslahi na ustawi wa walimu ipasavyo ili waweze kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi.

7.5.9. Ihakikishe kuwa kuna maduka maalum kwa ajili ya sare, viatu na mahitaji mengine ya wanafunzi.

7.5.10. Ihakikishe kuwa shule zote zina Siku ya Wazazi.

7.5.11. Iendelee kutekeleza kwa ukamilifu Sera ya Elimu ya Watu Wazima hasa Kisomo Chenye Manufaa na Elimu ya Kujiendeleza ili kuondoa ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu na ukosefu wa elimu kwa baadhi ya wazazi.

### 7.6 *Wajibu wa Jumuiya ya Wazazi*

7.6.1. Iwaelimishe na kuwahimiza wazazi na jamii kwa jumla kuhusu majukumu yao juu ya malezi ya watoto, shule na uhusiano wao na walimu.

7.6.2. Iwahimize wazazi kuhudhuria kwa ukamilifu Kisomo chenye Manufaa, Elimu ya Kujiendeleza, Mafunzo ya Elimu ya Afya



Digitized by Google

kwa familia na kutekeleza shughuli zote za maendeleo kwa jumla.

7.6.3. Ieleze, ifafanue na isimamie kwa ukamilifu utekelezaji wa Sera hii ya Malezi ya Taifa.

## 7.7. *Wajibu wa Wizara Inayohusika na Viwanda na Biashara na Wizara Inayohusika na Utalii na Maliasili*

**7.7.1. Wizara inayohusika na Biashara na Viwanda itahakikisha kuwa vifaa vya shule pamoja na nguo za watoto, viatu na vitambaa vya sare za shule vinapatikana na kudhibiti bei zake ili wazazi wamudu kuvinunua.**

7.7.2. Wizara hii pia ianzishe utaratibu maalum wa kuwa na maduka ya vifaa vya watoto wa shule.

**7.7.3. Wizara inayohusika na Utalii na Maliasili iwe na programu maalum ya kuwawezesha wanafunzi kutalii sehemu mbalimbali nchini.**

## 7.8. *Wajibu wa Taasisi Nyinginezo na Jumuiya mbalimbali Kuhusu Malezi ya Watoto*

Jamii ni pamoja na vikundi vya watu au Taasisi mbali mbali kama vile Polisi, Mgambo, Jeshi la Ulinzi na la Kujenga Taifa, Magereza, Zimamoto, Viongozi wa Chama na Serikali, Viongozi wa Madhehebu ya Dini, Wafanyakazi Viwandani, Relini, Bandarini, Hospitalini, n.k. Makundi yote haya yana wajibu mkubwa katika malezi ya watoto kwa hiyo yanapaswa kufanya yafuatayo:

7.8.1. Wawe mfano mzuri kwa watoto kwa kuwa na heshima, adabu, utii, upendo na ushirikiano, usafi wa mwili, mavazi na mazingira, unaghifu wa lugha, bidii na uhodari wa kazi.

7.8.2. Wasimamie kwa ukamilifu nidhamu ya watoto popote wawaonapo kwa kuwahimiza kuwa na adabu na heshima kwa wakubwa na kati yao wenyewe kwa wenyewe.

7.8.3. Kuwasaidia ili waepukane na ajali na kuwakemea wengine wanapotenda maovu.



Digitized by Google

7.9. ***Wajibu wa Viongozi wa Chama na Serikali***

Wawe mfano wa wazazi bora katika kutekeleza yote yaliyofafanuliwa katika Sera hii kuhusu wajibu wa watu wazima, wazazi na viongozi.

7.10. ***Wajibu wa Serikali za Miji na Vijiji***

7.10.1. **Serikali za Miji zifungue na kutunza viwanja vya kuchezea watoto mijini.**

7.10.2. **Serikali za vijiji zifungue viwanja hivyo vijijini.**

Digitized by Google

SURA YA TATU

# MALEZI YA VIJANA WA UMRI WA MIAKA 15—25

8.0. Hali ya Ujana na Mahitaji Yake

9.0. Malezi ya Vijana Nyumbani, Shuleni, Vyuoni, JKT na JKU

10.0. Malezi ya Vijana Mijini

11.0. Malezi ya Vijana Vijijini

12.0. Elimu ya Familia

13.0. Ndoa kwa Vijana

## 8.0. Hali ya Ujana na Mahitaji Yake

8.1. Kwa madhumuni ya Sera hii ya Malezi, kipindi cha ujana kimechukuliwa kuwa kati ya miaka 15 hadi 25.

8.2. Katika umri huu, vijana watakuwa wamemaliza elimu yao ya msingi. Walio wengi watakuwa nyumbani kwao; vijijini au mijini. Wachache watakuwa wamebahatika kuendelea na masomo; kwa hiyo watakuwa katika shule za Sekondari, Taasisi au Vyuo vya Mafunzo ya Kazi, Vyuo Vikuu, JKT na JKU au watakuwa ndio kwanza wameajiriwa na kuanza kazi. Wengine watakuwa wameoa au kuolewa na kuzaa watoto.

8.3. Katika kipindi cha ujana binadamu hupitia mabadiliko mengi ya kasi na mfululizo kwa mwili, akili, maono, haiba na kwa jamii, Ni kipindi cha mpito ambapo mtu huondokana na utoto na kuingia kwenye utu uzima. Kwenye utoto hayuko na kwenye utu uzima hayuko. Baadhi ya mambo ya utoto bado anayo na n mbo ya utu uzima yanaanza kumjia kwa hiyo nayo anayo pia. Kwa jumla kijana anaishi katika ulimwengu wa "kuwili".



Digitized by Google

8.4. **Ni kipindi ambapo kijana hana uhakika wala msimamo ulio thabiti isipokuwa kuyumba. Lakini maungo ya mwili wake na akili yake yamekua kiasi cha kutosha tayari kwa kumudu wajibu na majukumu ya utu uzima. Kwake ni kipindi kigumu** ambapo anakabiliwa na tatizo la uamuzi wa lipi linafaa kufanya na lipi halifai kufanya; lakini uwezo wa kufanya lolote kati ya hayo anao. Kwa hiyo anachohitaji ni msaada **wa malezi kutoka** kwa wakubwa,. wazazi, walimu na jamii kwa jumla ili apate ushauri na maelekezo sahihi. Akipata msaada huo anaweza kuwa na msimamo thabiti na wenye kuaminika.

8.5. Ili waweze kuwapa vijana msaada wa malezi, maelekezo na ushauri ipasavyo, watu wazima, wazazi, walimu na jamii, lazima kwanza wajue hali ya mabadiliko waliyo nayo vijana pamoja na mahitaji yao ya ukuaji. Kwa kawaida hali za vijana na mahitaji yao ya ukuaji ni kama ifuatavyo:

8.5.1. Katika kipindi hiki kijana anapata mabadiliko ya haraka sana ya kukua kwa mwili, yaani mifupa na viungo vyake vyote vya mwili na ana nguvu nyingi. Ukuaji huu wa haraka wa mwili unahitaji mambo yafuatayo:

(1) Chakula kingi na kilicho bora; hasa cha aina ya protini na wanga.

(2) Shughuli nyingi sana za kutumia viungo vya mwili kama vile michezo, ngoma, kulima, kutunza mifugo, useremala n.k. ili atumie nguvu alizo nazo. Katika kipindi hiki wakipewa mipango na maelekezo bora vijana wanaweza kutumika vizuri katika uzalishaji mali.

8.5.2. Ukuaji wa akili nao, kwa vijana walio wengi, hufikia kilele chake. Kwa hiyo hali ya kujiamini inakuwa kubwa zaidi. Wanataka fursa ya kubuni, kutafakari na kugundua ukweli wa mambo wao wenyewe.

8.5.3. Ukuaji wa mwili na akili walioufikia na hali ya kujiamini waliyo nayo, huwafanya vijana kuwa jasiri, shupavu na kupenda kujitokeza mbele kwa kila jambo. Ni wakati mzuri wa kuwapatia maandalizi ya kijeshi na ulinzi wa nchi, ubingwa katika michezo n.k. Ni wakati mzuri pia wa kuwafunza kazi zinazohitaji nguvu na ustamilivu.



Digitized by Google

8.5.4. Kwa sababu ya shughuli nyingi za mwili wanazozifanya, vijana pia wanahitaji mapumziko na burdani.

8.5.5. Vipaji vya mtu huanza kuonekana tangu wakati wa kipindi cha utoto lakini ni wakati wa kipindi hiki cha ujana ndipo vinajitokeza na kuonekana kwa wazi zaidi. Visipoendelezwa katika wakati huu vinatoweka.

8.5.6. Maendeleo ya hali ya uume (kwa watoto wa kiume) na ya hali ya uke (kwa watoto wa kike) pia yanafikia kilele, tayari kwa ajili ya kuchukua wajibu wa uzazi, yaani ubaba na umama. Kwa hiyo vijana wa kiume na wa kike wanavutiana na kutamaniana kwa mapenzi. Wanahitaji Elimu ya Familia ili wawe na maelekezo sahihi kuhusu wajibu wa uzazi na ili wajiheshimu.

8.5.7. Katika kipindi hiki pia vijana hupenda sana kuonekana kuwa wanapendeza na wenye hadhi katika jamii. Kwa hiyo hutamani vitu vizuri vinavyovutia na vya fahari.

8.5.8. Vijana wanapenda sana kujihusisha katika shughuli za ustawi wa jamii katika vikundi wanapokuwa shuleni, vyuoni, JKT, JKU, vijijini na mijini, kwa hiyo hupendelea sana kujiunga na timu za michezo, vilabu na vyama mbali mbali. Hupenda mambo ya starehe, ngoma, muziki, n.k. Huu ni wakati mzuri wa kuwaendeleza vijana katika michezo na utamaduni wa taifa kwa jumla.

8.5.9. Wanapenda sana watu wazima, wazazi, walimu na viongozi wakubaliane nao katika shughuli na mipango yao na kuzisifu shughuli hizo. Kwa jumla hawapendi kulaumiwa; wakisahihishwa wanajihisi vibaya. Hawapendi kujihisi wamekosea.

8.5.10. Wanapenda sana kupewa madaraka ya kuendesha shughuli zao wao wenyewe bila ya kuingiliwa na wakubwa, wazazi, walimu au viongozi. Hii ni kwa sababu vijana daima hujihisi wanao uwezo kamili wa kuendesha mambo yao wenyewe na pia kwa sababu huwaona watu wazima kama watu ambao wakati wao umepita na hivyo ni kipingamizi tu.



Digitized by Google

8.5.11. Pamoja na kupenda kuwa na uhuru wa kujifanyia na kuendesha mambo yao wao wenyewe, wanapokwama tu, wanataka na kukubali msaada na maelekezo ya watu wazima, wazazi, walimu au viongozi.

8.6. Hawapendi watu wazima, wazazi, walimu au viongozi wawaelekeze na kuingilia mambo yao lakini upendo, huruma na misaada yao wanaitaka. Hawapendi kubeba wajibu lakini wanadai haki.

8.7. Hudhani wanajua mengi, lakini ghafla wanajikuta hawajui kiasi cha kutosha kuwawezesha kutatua matatizo yao. Wanapenda kuyatawala na kuyaendesha wenyewe maisha yao lakini wanakuta kuna vikwazo vinavyowakwamisha. Kwa sababu hiyo, leo kijana anaweza akawa mkaidi, mbishi, asiyeshikika na asiye na ushirikiano lakini kesho akawa na hali ya unyenyekevu, mwema na mwenye ushirikiano mzuri.

8.8. Kwa upande mwingine watu wazima nao huwaona vijana kama watu wakaidi, wasiopenda kuelekezwa, wasio na ujuzi, uzoefu wala uwezo wowote. Kwa hiyo hawapaswi kusikilizwa wala kushirikishwa kwa namna yoyote isipokuwa kupewa amri na kulazimishwa. Huu si mtazamo sahihi.

8.9. Kijana pia hupenda kutambuliwa kwa nafsi yake na vitendo vyake kama mtu binafsi. Kwa hiyo katika kuwalea vijana, ni vyema pia watu wazima, wazazi, walimu na viongozi kumtazama kijana mmoja mmoja ili kufahamu hulka zake, vipaji vyake, shauku na matatizo yake ili kuweza kumsaidia katika kumuendeleza, kumrekebisha au kutatua matatizo yake.

## 9.0 Malezi ya Vijana Nyumbani, Shuleni, Vyuoni, JKT na JKU

### 9.1. *Wajibu wa Wazazi, Walimu na Viongozi wa Makambi*

9.1.1. Wajibu wa kwanza kabisa wa wazazi nyumbani, walimu katika shule za Sekondari na Vyuo na Viongozi wa Makambi ya JKT na JKU na taasisi nyingine zozote ambazo zinalea vijana, ni kufahamu hali za kimaumbile walizo nazo vijana na mahitaji yao ya kukua kama yalivyokwisha fafanuliwa.


Digitized by Google

9.1.2. **Popote walipo, nyumbani, katika shule za Sekondari, Vyuoni na makambini, wazazi, walimu na viongozi wahakikishe kuwa vijana wanapata chakula kingi na kilicho bora.**

9.1.3. Wawapatie vijana shughuli za kutosha za kufanya kila wakati kwa kutumia viungo vyao vya mwili na akili; wasikae bure hata kidogo. Shughuli hizo ziwe zenye manufaa na ziwe zimepangwa kwa utaratibu mzuri na ziwawezeshe vijana kujifunza na kuendeleza stadi na utaalam mbali mbali.

9.1.4. Wazazi nyumbani, walimu shuleni na nyuoni, na viongozi makambini wahakikishe kuwa vijana wanapata mapumziko, burdani na viburudisho vya kutosha baada ya shughuli zao.

9.1.5. Wawagawie vijana madaraka ya kufanya au kusimamia kazi maalum, mmoja mmoja au kwa vikundi, ili waanze kuwajibika. Kwa mfano kijana anaweza kupewa madaraka ya kutunza maktaba, mwingine akapewa kutunza bohari ya vifaa au ya chakula na mwingine kuangalia banda la kuku. Shamba la shule au la kambi linaweza kugawanywa katika vitalu kadhaa na kila kitalu kikakabidhiwa kwa kikundi maalum cha vijana wakitunze.

9.1.6. Nyumbani, shuleni, vyuoni au kambini, daima kuwe na sheria, taratibu, ratiba na mipango mizuri ya uendeshaji inayoeleweka, ili kila wakati vijana waelewe nini wanatakiwa kufanya na wapi wanatakiwa kuwepo. Mabadiliko yoyote katika utaratibu, ratiba na mipango iliyokwishaeleweka kwa vijana lazima yatolewe taarifa mapema. Wazazi, walimu na viongozi wa makambi wasiwe wanatoa amri au maelekezo yanayogongana yenyewe kwa yenyewe. Pawe na utaratibu maalum na madhubuti wa kupashana taarifa.

9.1.7. Wazazi, walimu na viongozi wa makambi wawe imara katika kusimamia na kuhakikisha kuwa vijana wanafuata sheria na taratibu zilizowekwa.

9.1.8. Katika shule za Sekondari na Vyuoni, vijana wawe na uongozi wao na viongozi wao waliowachagua kwa njia ya demokrasi.

9.1.9. Walimu wawashirikishe vijana, kwa kupitia Serikali yao na viongozi wao, katika uamuzi na upangaji wa mambo yote na



Digitized by Google

mipango yote inayohusu maisha yao. Wawajulishe mafungu ya fedha yaliyotolewa na Serikali kwa shule au chuo kwa ajili ya chakula, vifaa n.k. na wawashirikishe katika kupanga matumizi yao kama vile chakula cha aina gani na vifaa vya aina gani vinunuliwe kulingana na mafungu yaliyopo n.k.

9.1.10. Vijana lazima washirikishwe kwa ukamilifu katika mauzo ya mali au bidhaa walizozalisha shuleni, chuoni au kambini, wajue mapato na matumizi ya mapato hayo kwa wao wenyewe kushirikishwa katika uamuzi wa matumizi hayo.

9.1.11. Wazazi na walimu shuleni na vyuoni daima wawe na ushirikiano mzuri na vijana. Pia wawe na mtazamo wa kuelekeza na kushauri zaidi kuliko mtazamo wa kutawala, kuamuru na kulazimisha kila wakati.

9.1.12. Wazazi, walimu na viongozi makambini wawe wavumilivu katika kusikiliza na kupokea mchango wa mawazo wa vijana. Pia waheshimu na kuthamini utu wa vijana hao.

9.1.13. Wawalinde dhidi ya madhara, maadui na magonjwa.

9.1.14. Wajaribu kuwatia moyo kwa kila jambo zuri wanalofanya na kila wakati wawahimize na kuwakumbusha wawe na bidii katika kazi, michezo na shughuli za utamaduni, pamoja na bidii ya kujifunza kwa ukamilifu na tabia ya kulitafakari jambo kwa makini kabla ya kulitolea maoni.

9.1.15. Wawasaidie vijana katika kuwaepusha na marafiki wabaya na tabia mbaya za ulevi, uvutaji wa bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.

9.1.16. Walimu shuleni na vyuoni na wazazi nyumbani wawe na muda na utaratibu maalum wa kutoa mawaidha na ushauri kwa kijana mmoja mmoja kuhusu maendeleo yake kwenye masomo na shughuli nyinginezo shuleni, vipaji vyake vinavyofaa kuendelezwa, mwenendo wake na kazi inayomfaa achague baada ya kumaliza mafunzo.

9.1.17. Wawe na utaratibu mzuri wa kuonya na kuadhibu vijana kwa madhumuni ya kujenga tabia zao.



Digitized by Google

**9.1.18.** **Walimu shuleni na vyuoni wawe wanatoa taarifa kwa wazazi kuhusu maendeleo ya vijana, afya zao na vipaji vyao.**

**9.1.19.** **Wazazi nyumbani wawe na wakati wa kuzungumza na vijana ili kuelewa matatizo yao na ili kuwapa wasia na masimulizi mbali mbali ya mafunzo ya maisha.**

**9.1.20.** **Kwa jumla wazazi, walimu na viongozi makambini waonyeshe mfano wa maadili mema na maisha ya Ujamaa na Kujitegemea kwa vijana.**

**9.1.21.** **Wazazi, walimu shuleni na vyuoni na viongozi wawe mfano mzuri wa ushirikiano mzuri kati yao wenyewe kwa wenyewe. Wasigombane, kubishana au kuonyesha tofauti na migongano yao mbele ya vijana.**

9.1.22. Wazazi wawatimizie ipasavyo watoto na vijana mahitaji yao ya shuleni na wawe wanawasiliana nao mara kwa mara kwa njia ya barua n.k. ili kudumisha mshikamano wa familia.

9.1.23. Wazazi wawapatie vijana shughuli ndogo ndogo za uchumi zilizo zao wenyewe kama vile bustani, kufuga n.k. ili wajizalishie mali na kuanza kujitegemea kwa baadhi ya matumizi yao.

## 9.2. *Malezi ya Vijana Katika Shule za Sekondari*

9.2.1. Walimu katika shule za sekondari wanapaswa kutekeleza kwa ukamilifu yale yote yaliyokwisha fafanuliwa kuhusu wajibu wa wazazi, walimu na viongozi wa makambi.

9.2.2. Elimu ya Sekondari inayotolewa kwa vijana lazima iwe iliyokamilika katika kila fani ili ijenge msingi mzuri wa kupatia wataalam wetu. Ili kufikia lengo hili shule za Sekondari lazima ziwe na walimu wa kutosha, vifaa vya kutosha na mitaala inayokazia ufundi, stadi, sayansi na teknolojia mbali mbali.

9.2.3. Elimu ya Kujitegemea lazima itekelezwe kwa ukamilifu. Kwa hiyo yafuatayo yatiliwe maanani:

(1) Kazi iwe in sehemu ya elimu na vijana wawe wanazalisha mali ili shule yao ijitegemee kwa chakula na vifaa.



Digitized by Google

(2) Njia za kufundishia ziwe:

(a) Njia za uvumbuzi

(b) Zinazowapa vijana shughuli na vitendo halisi.

(c) Zinazowapa vijana shughuli za kufanya mmoja mmoja na katika vikundi.

(3) Shule iwe sehemu ya jamii. Vijana na walimu washiriki katika shughuli za maendeleo katika jumuiya inayoizunguka shule na jumuiya ishirikishwe katika shughuli za maendeleo na ustawi wa shule na ijifunze utaalam kutokana na shughuli zilizopo shuleni.

9.2.4. Elimu ya Siasa ifundishwe kwa makini ili vijana wajue wajibu wao na haki zao kulingana na Siasa ya nchi. Wajue pia uhusiano wa nchi yao na nchi nyingine katika bara la Afrika na Ulimwengu kwa jumla.

9.2.5. Kuwepo vikundi na vilabu mbali mbali shuleni ambavyo vijana wanaweza kujiunga ili kuendeleza vipaji vyao kama vile vikundi vya majadiliano na kongamano, kwaya, vikundi vya utamaduni na ngoma, skauti wa kiume na wa kike.

9.2.6. Kuwepo Tawi la CCM, Tawi la Umoja wa Vijana na Matawi ya Jumuiya nyingine za Wananchi ili vijana, walimu na watu wengine waliopo shuleni waweze kijiunga na kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli za kisiasa.

9.2.7. Vijana wahimizwe kujifunza kwa makini na kwa bidii.

9.2.8. Katika shule za Sekondari kuwepo walimu washauri wa kuwapa mawaidha na ushauri vijana kuhusu kazi zinazowafaa wamalizapo masomo na pia kuhusu mbinu za kupambana na matatizo ya maisha.

9.2.9. Kila shule ya Sekondari inapaswa kuwa na mwelekeo wa kuimarisha vijana wanaosoma hapo katika taaluma, fani, au stadi fulani maalum, na iweze kuwa na sifa katika taaluma, fani au stadi hiyo. Vijana watajivunia jambo hili kwa muda mrefu maishani mwao na litasaidia kudumisha mshikamano wa tabia.



Digitized by Google

9.2.10. **Vijana wote, wapate mafunzo ya Elimu ya Familia ili waweze kukabiliana na mabadiliko ya ukuaji wao.**

9.2.11. **Vijana wafanye kazi vijijini wakati wa likizo.**

### 9.3. *Malezi ya Vijana Katika Vyuo*

9.3.1. Walimu katika vyuo, vyuo vikuu na taasisi nyinginezo za mafunzo ya juu wanapaswa kutekeleza kwa ukamilifu yote yaliyokwisha fafanuliwa kuhusu wajibu wa wazazi, walimu na viongozi wa makambi katika Sera hii.

9.3.2. Elimu ya Kujitegemea itekelezwe kwa ukamilifu kama ilivyokwisha fafanuliwa katika kipengere kinachohusu elimu ya Sekondari katika Sera hii.

9.3.3. Elimu ya Siasa pia ifundishwe kwa ukamilifu ili vijana wajue wajibu wao na haki zao kulingana na siasa ya nchi na ili wajue uhusiano wa nchi yao na nchi nyingine katika bara la Afrika na ulimwenguni kwa jumla.

9.3.4. Mafunzo ya taaluma na mafunzo ya kazi yasiwe ya nadharia tu bali yahusiane na vitendo halisi na hali halisi ya mazingira ambayo vijana watakwenda kufanya kazi na kuishi.

9.3.5. Vijana wapate fursa ya kufanya kazi katika mazingira halisi wanayotarishiwa kwenda kufanyia kazi kama vile vijijini, katika idara za Serikali, Mashirika n.k. wakati wa likizo.

9.3.6. Vyuo, Vyuo Vikuu na Taasisi nyinginezo za mafunzo ya juu viwe ni chimbuko la utafiti kuhusu fani mbali mbali za masuala ya maendeleo ya taifa na mapinduzi kwa jumla ili kuvumbua mbinu bora zaidi za kusukumia maendeleo na mapinduzi hayo.

9.3.7. Walimu vyuoni wawe na wakati maalum wa kutoa ushauri na mawaidha kwa vijana.

9.3.8. Vijana wajifunze kufanya uchambuzi na tafsiri ya mambo mbali mbali katika [illegible] kuhusu uchumi, siasa, itikadi na maendeleo kwa jumla.



Digitized by Google

9.3.9. Masomo ya ufundi, sayansi na teknolojia yapewe umuhimu wa pekee na yafundishwe kwa makini.

9.3.10. Matawi ya Chama, Umoja wa Vijana, Umoja wa Wanawake na Jumuiya nyinginezo za wananchi yafunguliwe na kuimarishwa ipasavyo katika vyuo.

9.3.11. Vyuo viwatayarishe vijana kwa maisha yao binafsi kwa kuwapa maelekezo sahihi kuhusu matumizi mazuri ya mshahara, marafiki wanaofaa, matatizo yatokanayo na ulevi, uvutaji na anasa za kupita kiasi na wajibu wao katika kusaidia wazazi na ndugu zao.

**9.4. *Wajibu wa Wizara ya Elimu, Wizara Nyingine na Mashirika Yenye Vyuo na Shule za Sekondari***

9.4.1. Wizara ya Elimu itaendelea kuandaa mitaala na mihutasari itakayotumika kwa shule zote za Sekondari na Vyuo vyote nchini. Vyuo Vikuu na Taasisi nyingine zinazojitegemea zitaandaa mitaala na mihutasari yao wenyewe lakini lazima ilingane na mahitaji ya Taifa.

9.4.2. Wizara ya Elimu, Wizara nyingine, Mashirika na Jumuiya zenye Vyuo, Taasisi na shule za Sekondari zinapaswa kufanya yafuatayo:

(1) Kuhakikisha kuwa Vyuo, Taasisi na shule za Sekondari wanazoziendesha zina vifaa vya kutosha na walimu/wakufunzi wa kutosha na kwamba walimu/wakufunzi hao wamehitimu ipasavyo na mienendo yao inalingana na mahitaji ya taifa letu.

(2) Wanafunzi katika shule za Sekondari, Vyuo, Vyuo Vikuu na Taasisi wanazoziendesha wanapata chakula cha kutosha na kilicho bora.

(3) Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Elimu ya Kujitegemea katika shule za sekondari, Vyuo, Vyuo Vikuu na Taasisi hizo.

(4) Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Sera hii ya



Digitized by Google

Malezi ya Taifa katika shule, Vyuo na Taasisi wanazoziendesha.

9.4.3. **Kuhakikisha kuwa kunakuwepo utaratibu maalum wa kutoa** motisha kwa walimu na wakufunzi kwa kuwapa maslahi, hali za kazi zinazoridhisha na mahali pazuri pa kuishi, kulingana na majukumu waliyo nayo.

9.4.4. Kuwa na programu za kuendeleza shule za Sekondari, Vyuo, Vyuo Vikuu na Taasisi katika fani mbali mbali kitaaluma na kijamii.

**9.5. Wajibu wa Wizara Inayohusika na Mambo ya Kazi na Utumishi**

9.5.1. Itahakikisha kuwa vijana wanaomaliza mafunzo kwenye vyuo na taasisi za kusomea kazi wanapangwa kwenye kazi walizozisomea.

9.5.2. Itahakikisha kuwa kuna utaratibu wa kuwaelekeza na kuwafuatilia vijana mpaka wanapoimarika kazini.

9.5.3. Itahakikisha kuwa kuna misaada mbali mbali ya kuwawezesha vijana wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza kuanza maisha vizuri. Misaada hiyo ni kama vile mikopo n.k.

***9.6. Wajibu wa Waajiri na JUWATA Kuhusu Vijana Wanapoajiriwa***

9.6.1. Waajiri lazima wawape mwongozo na maelekezo vijana wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza kuhusu:

(1) Mwenendo bora wa maisha wanaopaswa kuwa nao kazini na nje ya kazi.

(2) Sheria za msingi na kanuni za kazi zinazotawala haki na wajibu wao.

(3) Maelezo ya shughuli wanazotarajiwa kufanya katika kazi au madaraka waliyopangiwa.

(4) Athari za ulevi, uvivu na uzembe kazini.



Digitized by Google

(5) Wajibu wa kuwasaidia wazazi na ndugu zao na umuhimu wa kwenda nyumbani wakati wa likizo.

9.6.2. Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania (JUWATA) inapaswa kusimamia kwa dhati wajibu na haki za wafanyakazi na kukosoa wafanyakazi wabovu katika sekta zote ili wasiwe mfano mbaya kwa vijana wanaoajiriwa.

## 10.0. Malezi ya Vijana Mijini na Vijijini

### 10.1. *Mambo Yanayoathiri Malezi ya Vijana Mijini*

10.1.1. Kuwepo kwa mkusanyiko na mchanganyiko wa desturi nyingi zinazotofautiana kwa sababu ya kuwepo kwa watu kutoka kwenye jamii mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kwa sababu ya mchanganyiko huo wa desturi kunakuwa hakuna mfumo mmoja wa desturi unaofuatwa na watu wote na matokeo ni vurugu ambayo inapotosha vijana kimaadili.

10.1.2. Kuwepo kwa mkusanyiko wa watu wengi wenye tabia na hulka mbali mbali za kutenda matendo ambayo huigwa na vijana.

10.1.3. Ukosefu wa kazi na shughuli maalum za uchumi, jambo ambalo husababisha baadhi ya watu kujiingiza katika vitendo vya wizi, ujambazi, lugha chafu n.k. ambavyo huigwa na vijana.

10.1.4. Kuwepo kwa vyombo vya starehe na uenezi kama vile sinema, video, televisheni na magazeti ambayo hutumika kwa kueneza tabia, matendo na desturi mbaya.

10.1.5. Kutokuwepo kwa burdani na shughuli za starehe zinazowafikia watu wote kwa usawa kwa sababu ya burdani nyingi mijini kuendeshwa kwa misingi ya biashara na hivyo wengi hushindwa kuzimudu.

10.1.6. Kuna upungufu wa nyumba mijini; na hizo chache zilizopo hazina nafasi za kutosha. Jambo hili husababisha baadhi ya vijana na hata watu wazima kutokuwa na mahali pa kuishi penye uhakika.



Digitized by Google

## 10.2. *Mambo Yanayoathiri Malezi ya Vijana Vijijini*

10.2.1. Kutokuwepo kwa mipango thabiti ya kuwapokea vijana wanaomaliza shule za msingi na kuwaingiza katika shughuli za uchumi zenye manufaa kwao wenyewe na kwa jamii yao.

10.2.2. Ukosefu wa huduma muhimu za jamii kama vile maji, umeme, barabara, hospitali, nguo za kutosha, nyumba bora za kuishi n.k.

10.2.3. Kutokuwepo kwa huduma mbali mbali za burdani kama vile majumba ya starehe, sinema, televisheni, muziki n.k.

10.2.4. Ukosefu wa teknolojia, pembejeo na zana bora za kufanyia kazi, jambo ambalo husababisha kazi vijijini (kilimo, ufugaji, uvuvi n.k.) kuwa ngumu na zisizotoa mazao ya kutosha.

10.2.5. Wazazi kutokuwa na utaratibu wa kuwapa vijana sehemu ya mapato yanayotokana na kazi walizofanya kwa pamoja na vijana wao ili wajitegemee.

10.2.6. Mambo yaliyoelezwa hapo juu husababisha vijana wengi kukimbilia mijini kufuata huduma za jamii zilizo bora zaidi na kutafuta kazi za ajira. Wanapokosa kazi wanazagaa ovyo na kujiingiza katika vitendo viovu, katika jitihada yao ya kujaribu kumudu maisha ya mjini.

## 10.3. *Wajibu wa Serikali na Wizara mbalimbali Kuhusu Malezi ya Vijana Mijini na Vijijini*

10.3.1. Serikali na Wizara zinazohusika na Ujenzi, Usafiri, Kilimo na Mifugo, Biashara na Viwanda, Nishati, Ardhi, Maliasili, Afya, Maendeleo ya Jamii na Utamaduni, Ushirika n.k. pamoja na Serikali za Mitaa na Serikali za Vijiji, zihakikishe kuwa yafuatayo yanafanyika:

(1) Vijiji vinapatiwa huduma bora za jamii, kama vile maji safi na ya kutosha, barabara, usafiri, hospitali, dawa, umeme, nguo, vifaa vya ujenzi wa nyumba bora n.k.

(2) Vijiji vinapatiwa maarifa, pembejeo na vyombo bora vya



Digitized by Google

kufanyia shughuli za uchumi katika kilimo, ufugaji, uvuvi n.k.

(3) Shughuli za viwanda vidogo vidogo zinaanzishwa, kuimarishwa na kupanuliwa vijijini na mijini.

(4) Ushirika wa uzalishaji mali unaanzishwa na kupanuliwa kila mahali vijijini.

(5) Kuna mipango madhubuti ya kuwapatia wananchi vijijini burdani baada ya saa za kazi, kama vile sinema, michezo n.k. na kunajengwa majumba ya maendeleo na starehe.

(6) Vijiji viwe na mipango maalum ya kuwapokea na kuwatumia ipasavyo vijana wanaomaliza elimu ya msingi kama vile taifa lilivyo na mipango maalum kwa vijana wanaomaliza Elimu ya Sekondari na Vyuo.

(7) Kuanzishwe Jeshi la Kujenga Vijiji kwa vijana waliomaliza Elimu ya Msingi ili wajifunze kulihudumia taifa na vijiji vyao kabla hawajaanza kujitegemea.

10.3.2. *Wajibu wa Wizara inayohusika na Maendeleo ya Jamii, Utamaduni na Vijana*

(1) Wizara inayohusika na Maendeleo ya Jamii, Utamaduni na Vijana ihakikishe kuwa kuna burdani na starehe inayowafikia wananchi walio wengi mijini na vijijini.

(2) Iwaunganishe vijana na watu wazima, mijini na vijijini, katika vikundi mbali mbali vya sanaa za maonyesho, ngoma n.k. ili wajiburudishe baada ya kazi na ili kuendeleza utamaduni wa taifa.

10.3.3. *Wajibu wa Halmashauri za Miji*

Halmashauri za miji zifungue majumba ya utamaduni mijini ambako sanaa za maonyesho, ngoma n.k. zitachezwa kama burdani na pia ifungue bustani na viwanja vya kupumzikia watu.

10.3.4. *Wajibu wa Wizara Inayohusika na Habari na Utangazaji*

(1) Ihakikishe kuwa magazeti, filamu, picha, video na



Digitized by Google

michezo ya televisheni inayoingizwa kutoka nje au kutengenezwa hapa nchini inasaidia kuendeleza na siyo kuvuruga maadili, utamaduni na uchumi wa taifa letu.

(2) Kwa kutumia idara zake na mashirika inayoyaongoza, Wizara hiyo ieneze malezi bora ya Taifa.

10.3.5. *Umuhimu wa Televisheni*

Serikali ya Jamhuri ya Muungano ianzishe televisheni Tanzania Bara ili isaidie katika kujenga maadili ya vijana na kusukuma maendeleo ya jamii.

10.3.6. *Wajibu wa Kampuni ya Filamu Tanzania*

Iandae filamu zitakazochukua nafasi ya zile filamu za kigeni zinazoonyeshwa sasa ambazo hazilingani na matarajio yetu. Filamu za kampuni hii zikidhi mambo yafuatayo:

(1) Kuendeleza utamaduni na maadili mema na kutoa burdani nchini.

(2) Kuhimiza na kuelimisha wananchi juu ya shughuli za maendeleo ya uchumi na ya jamii kama vile kilimo cha kisasa, kanuni za afya, lishe, ujenzi wa nyumba bora n.k.

10.3.7. *Wajibu wa Wizara Inayohusika na Mambo ya Ndani na Wizara ya Sheria*

Kupambana kwa ukamilifu na watu wenye hulka mbaya ya uvunjaji wa sheria za nchi dhidi ya matendo maovu yanayoweza kuigwa na vijana, kama vile:

(1) Wizi, ujambazi na uzururaji.

(2) Ulevi wa kupindukia, uvutaji wa bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.

(3) Lugha mbaya.

(4) Kudhibiti saa za starehe kama vile dansi na kudhibiti utengenezaji na saa za unywaji wa pombe.

10.3.8. *Wajibu wa Wizara Inayohusika na Utalii na Maliasili*

(1) Kuandaa programu za kuwawezesha vijana kutembelea na kuona sehemu mbali mbali nchini kwa gharama nafuu.



Digitized by Google

(2) Kuwaelimisha vijana ili kuwafanya wathamini na kupenda maliasili kama vile ardhi, maji, mimea, wanyama, ndege na wadudu.

(3) Kuandaa programu za kuwashirkisha vijana katika shughuli za:

(a) Upandaji na utunzaji wa miti;

(b) Kuhifadhi na kutunza mazingira ya asili;

(c) Kuhifadhi na kutunza wanyama, wadudu na ndege.

**10.4. *Wajibu wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT)***

10.4.1. Iandae programu ya utekelezaji wa mambo yanayohusu wanawake katika malezi ya vijana.

10.4.2. Isimamie kwa ukamilifu uendelezaji wa shughuli za sayansi kimu nchini kama vile:

(1) Upishi bora wa vyakula mbalimbali;

(2) Kuendeleza vyakula vya jadi;

(3) Usafi wa mwili, mavazi na mazingira;

(4) Matunzo ya nyumba na familia.

**11.0. Wajibu wa Umoja wa Vijana Kuhusu Malezi ya Vijana**

Pamoja na kwamba Umoja wa Vijana unahusika na malezi ya watoto katika kila kipindi cha ukuaji wao, katika rika la vijana una sehemu muhimu zaidi hasa kwa vile umoja huu uko maalum kwa ajili ya vijana. Wajibu wa Umoja wa Vijana utakuwa kama ifuatavyo:

11.1. Ufungue, usimamie, na uimarishe Matawi ya Umoja huu na shughuli zake katika shule za Sekondari, Vyuoni, katika makambi ya majeshi, sehemu za kazi, vijijini na mijini.

11.2. Ubuni programu mbalimbali za uzalishaji mali kwa ajili ya vijana Mikoani, Wilayani, Vijijini na Mijini kwa kushirikiana na kuhusisha taasisi na vyombo mbali mbali vinavyohusika.



Digitized by Google

11.3. Uwaunganishe vijana katika vikundi Mikoani, Wilayani, Mijini na Vijijni, ambako kwa kushirikiana na wananchi wengine watatekeleza yafuatayo:

(1) Programu za uzalishaji mali kwa ushirika

(2) Shughuli za michezo, sanaa, utamaduni na burdani

(3) Uchambuzi na ufafanuzi wa Siasa, Itikadi, Uchumi na masuala ya maendeleo.

(4) Kuwajenga vijana kuwa imara katika kutekeleza, kulinda na kutetea maamuzi na maelekezo ya Chama na kuwa macho na kupinga jitihada za kupotosha utekelezaji wa maamuzi na maelekezo hayo.

(5) Kuwa na programu za kufundisha vijana ukakamavu, ujasiri, nidhamu, usafi, udadisi n.k.

(6) Kufanya kazi za kujenga taifa.

**12.0. Elimu ya Familia**

12.1. Zamani katika nchi yetu, jamii nyingi zilikuwa zinatoa mafunzo ya Elimu ya Familia kwa vijana yaliyojulikana kama "Jando na Unyago". Kwa sababu ya mabadiliko kadhaa, jamii zinazoendelea kutoa mafunzo haya hivi sasa ni chache na hata hizo mafunzo zinayotoa hayatoshi kuweza kutatua matatizo ya vijana kulingana na mazingira ya sasa. Isitoshe desturi ya baadhi ya jamii hizo ya kutahiri watoto wa kike katika unyago huhatarisha afya za vijana hao.

12.2. Kulingana na umuhimu wake kwa vijana, kuanzia sasa mafunzo ya Elimu ya Familia yatolewe kwa vijana wote wanapofikia umri huu kwa wakati maalum, mahali maalum na watu maalum.

12.3. Jamii zinazohusika ziache desturi ya kutahiri watoto wa kike. Njia za kuelimisha, kuelekeza na kushawishi zitumike katika kuzifanya jamii hizo ziachane na desturi hiyo.



Digitized by Google

12.4. Vyombo vyote vinavyohusika na malezi kama vile madhehebu ya dini, taasisi mbali mbali, wazee wa jadi n.k. watahusika kutoa mafunzo ya Elimu ya Familia kulingana na utaratibu utakaoandaliwa na Wizara ya Elimu.

**12.5. *Madhumuni ya Mafunzo ya Elimu ya Familia***

(1) Kuwawezesha vijana kukabili bila ya wasiwasi au mshangao mabadiliko yanayotokea katika miili yao na nafsi zao kwa jumla wakati wa kipindi cha ujana.

(2) Kuwatayarisha vijana kufahamu mambo ya utu uzima yanayohusu misingi ya ndoa na umuhimu wake katika uzazi, na wajibu wa kulea watoto katika mtazamo unaolingana na maadili ya taifa.

(3) Kuwapatia vijana wa kiume na wa kike msimamo wa kuweza kukaa pamoja na kufanya shughuli zenye manufaa kwao na kwa taifa lao kwa kujiamini, kushirikiana na kuheshimiana.

(4) Kuwaelimisha vijana kuhusu athari za kuzaa mapema na kuzaa nje ya ndoa kwa wao wenyewe, kwa watoto watakaowazaa na kwa jamii yao.

**12.6. *Muhtasari wa Elimu ya Familia na Umri wa Mafunzo***

12.6.1. Elimu ya Familia ifundishwe kwa vijana waliobalehe.

12.6.2. Wizara ya Elimu itaandaa muhtasari, utaratibu, vifaa na vitabu vya Somo la Elimu ya Familia, na walimu wa kufundisha somo hilo. Walimu watachaguliwa kutoka kwenye shule au jamii kulingana na uzoefu na ujuzi wao katika Elimu ya Familia na heshima waliyo nayo ili vijana waweze kuwaamini na kuwaiga.

**13.0. Ndoa kwa Vijana**

13.1. Katika kipindi hiki vijana huoa na kuolewa. Ili ndoa iweze kuwa na manufaa lazima idumu. Ndoa inayovunjika ina athari kwa malezi ya watoto waliyozaliwa katika ndoa hiyo, kwa wazazi waliyoachana na kwa jamii, kama itakavyofafanuliwa hapo mbele katika sera hii.



Digitized by Google

13.2. Ili ndoa iweze kudumu na iwe yenye maisha bora na ya manufaa, mambo yafuatayo yazingatiwe:

13.2.1. Vijana wanaooana wawe wanafahamiana kiasi cha kutosha.

13.2.2. Wapate idhini na baraka za wazazi au walezi wa pande zote mbili.

13.2.3. Wapate mawaidha na maelekezo ya wazazi, wazee au viongozi mbalimbali katika jamii kuhusu maisha ya ndoa.

13.2.4. Wote wawili, mke na mume, wazingatie ipasavyo uzazi wa majira na wapate mafunzo ya uzazi wa majira na malezi bora ya watoto.

13.2.5. Wote wawe na kazi maluum, ama ya ajira au ya binafsi kama vile kilimo, uvuvi, ufundi n.k. na wawe wanaifanya kwa utaalam, bidii na nidhamu ili kuhakikisha wana mapato ya kutosheleza kuendesha maisha yao na ya watoto watakaowazaa.

13.2.6. Wote wawe wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu na wawe wanajiendeleza katika elimu ili kujiongezea maarifa juu ya mazingira yao, ujuzi na utaalam wa kazi zao na wa malezi ya watoto wao.

13.2.7. Wawapende, wawaheshimu na kila inapobidi wawasaidie ipasavyo wazazi na ndugu wa pande zote mbili.



Digitized by Google

# FAMILIA, URITHI, WATOTO WA NJE YA NDOA NA WATOTO WASIO WA KAWAIDA

14.0. Umuhimu wa Familia katika Malezi

15.0. Urithi wa Mali ya Familia

16.0. Matatizo ya Watoto wa Nje ya Ndoa

17.0. Matatizo ya Watoto Wasio wa Kawaida

18.0. Mwisho

## 14.0. Wajibu wa Familia Katika Malezi

14.1. Familia ni baba, mama, watoto na ndugu wa karibu; na msingi wake mkubwa ni ndoa. Pamoja na yote yaliyokwisha elezwa kuhusu wajibu wa wazazi, familia ina kazi mbili muhimu ambazo ni kuongeza idadi ya watu na kuzalisha mali na chakula cha kutosha na kilicho bora.

14.2. Ili iweze kusimamia na kutekeleza kwa ukamilifu wajibu wake katika uzalishaji mali na chakula, kutunza na kulea vizuri watoto, mambo muhimu yafuatayo lazima yawepo katika familia:

14.2.1. Mahitaji ya kutosha kwa kila mmoja; kwa hiyo familia lazima iwe na utaratibu mzuri wa kufanya kazi.

14.2.2. Familia iwe na nyumba bora na yenye nafasi ya kutosha, iwe na afya ya mwili, akili, maono yaliyotengemaa na maadili mema yanayolingana na siasa ya nchi. Tukiwa na familia zilizo imara katika itikadi, siasa, uchumi, jamii, maono na katika maadili ya ujamaa, tutakuwa na taifa lililo imara.

14.2.3. Familia iwe na elimu, ujuzi, hekima na busara za kuiwezesha kumudu kazi na majukumu yake. Kila mtu ndani ya familia ajue



Digitized by Google

kusoma, kuandika na kuhesabu, na watoto wote wenye umri wa kwenda shule waende shule.

14.2.4. Viongozi wa familia wanapaswa kuelewa bara bara sheria, kanuni, mila na desturi zinazotawala mazingira na jamii wanamoishi ili waweze kuzifuata na kuwaelekeza wengine katika familia. Baba na mama wahakikishe kuwa wanatekeleza wajibu wao ipasavyo kwa watu wote waliomo katika familia zao.

## 15.0. Urithi wa Mali ya Familia

15.1. Mahitaji ya familia, ustawi na maendeleo yake katika elimu, afya, uchumi na mshikamano wake, hutegemea mali waliyo nayo kwa pamoja. Kwa hiyo urithi ni jambo la msingi sana katika suala la malezi ya watoto na vijana, kwa sababu linahusu umilikaji wa mali iliyozalishwa na familia, na ambayo ndiyo nguvu ya familia, baada ya mmoja au viongozi wote wa familia (baba au mama) kufariki.

15.2. Katika jamii zetu zilizo nyingi hivi sasa hakuna utaratibu wala mwenendo wa kufaa na wa kuaminika unaohakikisha kwanza kuwa mali inayozalishwa na familia ni ya familia kwa pamoja na sio ya mtu binafsi, baba au mama peke yake; pili endapo mmoja au viongozi wote wa familia wanafariki, mali ya familia inamilikiwa na familia kwa pamoja na kwamba inaendelea kutumika kwa ajili ya malezi ya watoto, maendeleo na ustawi wa familia hiyo.

15.3. Mara nyingi, ndugu hasa wa upande wa kiongozi wa kiume, baada ya kiongozi huyo kufariki, huvamia na kupora mali ya familia. Wakati mwingine pia, mmoja au baadhi ya watoto wachache wa marehemu au jamaa zake ndani ya familia yenyewe hupora na kuhodhi mali hiyo.

15.4. Vitendo vya namna hii husababisha watoto, vijana, jamaa, mama au baba waliokuwa wanalelewa, kutunzwa na kuendelezwa na mali hiyo, kuachwa bila ya msaada wowote na pia husababisha mfarakano na migongano ndani ya familia. Matokeo ni kwamba mshikamano wa familia huvunjika; watoto,



Digitized by Google

vijana na jamaa wa familia hiyo hutangatanga na kukosa matunzo na malezi bora.

15.5. Ili kurekebisha hali hii, mambo yafuatayo ni muhimu yafanyike:

15.5.1. Serikali itunge sheria yenye kuzingatia utaratibu unaotoa ufafanuzi ulio bora zaidi kuhusu umilikaji na urithi wa mali katika familia unaohakikisha kwamba:

(1) Mali inayozalishwa na familia ni ya familia kwa pamoja.

(2) Mmoja au viongozi wote wa familia (baba au mama) wanapofariki mali ya familia inarithiwa kwa namna ambayo itaendelea kuwa ni ya familia kwa pamoja na inatumika kwa maendeleo na manufaa ya watu wote wa familia hiyo.

15.5.2. Viongozi wa familia (baba au mama) wauelewe utaratibu huo utakaowekwa na sheria hiyo na wafanye maandalizi, kulingana na utaratibu huo, yatakayohakikisha kuwa baada ya mmoja au wote kufariki, mali ya familia inaendelea kutumika kwa ajili ya maendeleo ya familia yao.

## 16.0. Matatizo ya Watoto Walioko Nje ya Ndoa

**16.1.** ***Watoto walioko nje ya ndoa na matatizo yao, wanaweza kugawanywa katika makundi yafuatayo:***

16.1.1. Watoto waliozaliwa katika ndoa ambayo baadaye ilivunjika na hivyo kulazimika kuishi na kukulia kwa mmoja tu wa wazazi wao; baba au mama peke yake. Kama huyo mzazi anayeishi nao hana uwezo wa kutosha na hapati msaada wowote kutoka kwa mzazi mwenzie, watoto hawapati matunzo mazuri. Katika hali hii pia watoto huwa hawapati mapenzi yenye mshikamano wa wazazi wote wawili, na tukio lenyewe la kufarakana kwa wazazi wao linaweza kuwafanya wafadhaike. Haya yote yanaweza kuathiri vibaya ukuaji wa akili na maono ya watoto hao.

16.1.2. Watoto waliozaliwa na wazazi ambao hawajafunga ndoa na



Digitized by Google

ambao hawaishi pamoja na kwa hiyo kulazimika pia kuishi na mmoja tu wa wazazi wao. Hali kadhalika kama mzazi huyo hana uwezo wa kutosha na hapati msaada wowote kutoka kwa mzazi mwenzie, watoto hawawezi kupata matunzo mazuri. Pia hawawezi kupata mapenzi yenye mshikamano wa wazazi wote wawili.

16.1.3. Watoto wanaokulia katika ndoa ya pili ya baba au mama; yaani baada ya ndoa yake ya kwanza kuvunjika baba yao ameoa mke mwingine au mama yao ameolewa na mume mwingine. Watoto wa namna hii huenda wasikubalike na kupata upendo kwa ukamilifu kutoka kwa baba au mama wa kambo, ndugu wa kambo na ndugu watakaochangia baba au mama. Kwa watoto wa namna hii pia, ukuaji wao na malezi yao yatakuwa na dosari.

16.1.4. Watoto wanaozaliwa na wazazi ambao hawakuoana na baadaye mmoja wa wazazi hao kuoa mke ambaye sio mama wa watoto hao au kuolewa na mume ambaye siye baba wa watoto hao. Hali ya watoto itakuwa sawa sawa na wale wanaoishi katika ndoa ya pili ya baba au mama yao kama ilivyokwisha elezwa hapo juu.

16.1.5. Watoto ambao huzaliwa na wazazi ambao hawajaoana, wana umri mdogo na ambao hawaishi pamoja; kwa hiyo kulazimika kuishi na kulelewa na ama mmoja tu wa wazazi au na ndugu za wazazi hao. Wazazi wa namna hii hawajajiandaa kuweza kujitegemea, kwa hiyo wao na watoto waliowazaa watakuwa mzigo kwa ndugu zao. Vijana wanaozaa mapema mno huhatarisha afya zao kwa vile miili yao haijakomaa kiasi cha kutosha kuweza kumudu majukumu ya uzazi kwa ukamilifu.

**16.2. *Ili kusaidia tatizo la watoto wa nje ya ndoa mambo yafuatayo yafanyike***

16.2.1. Madhehebu ya dini, Jumuiya ya Wazazi, Jumuiya ya Wanawake na Idara ya Ustawi wa Jamii wawe na programu maalum za kutoa mawaidha kwa vijana na watu wazima mitaani, vijijini, viwandani, na shuleni, ili kupunguza mfarakano wa ndoa.

16.2.2. Taasisi zilizotajwa hapo juu wawape vijana ushauri utakaowawezesha kutoendelea kupata watoto nje ya ndoa.



Digitized by Google

16.2.3. Shuleni, makambini n.k. kuanzishwe mabaraza ya ushauri kwa ajili ya kuwashauri vijana na kuwasaidia wasipate watoto wa nje ya ndoa.

16.2.4. Madhehebu ya dini, Jumuiya ya Wazazi, Jumuiya ya Wanawake na Idara ya Ustawi wa Jamii wawaelimishe na kuwakumbusha wazazi kuhusu wajibu wao wa kuangalia maadili ya watoto na vijana wao.

## 17.0 Matatizo ya Watoto Wasio wa Kawaida

17.1. Watoto wasio wa kawaida ni pamoja na wale ambao ni walemavu wa viungo vya mwili, akili na maono; manunda ambao familia imeshindwa kuwalea na wale watoto ambao ni yatima.

17.2. Wakipewa malezi maalum na wakifanyiwa maandalizi mazuri, watoto wasio wa kawaida wanaweza kukua vyema na kuwa na manufaa kwao na kwa jamii. Mambo yafuatayo ni muhimu yafanyike:

17.2.1. Wizara ya Elimu iandae na kusimamia utaratibu wa kutoa elimu maalum kwa ajili ya watoto wasio wa kawaida ambao ni pamoja na kujenga shule maalum na kutayarisha mitaala maalum, walimu maalum, vitabu na vifaa maalum.

17.2.2. Wizara inayohusika na Viwanda na Biashara ihakikishe kuwa vifaa maalum kwa ajili ya elimu, malezi na matunzo ya watoto wasio wa kawaida vinapatikana, ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda vya kuweza kuvitengeneza vifaa hivyo nchini.

17.2.3. Wizara inayohusika na Ustawi wa Jamii ipanue na kuimarisha vituo vya kutunzia na kulelea watoto wasio wa kawaida pamoja na kuimarisha utaalam wa kutunza na kulea watoto hao nchini. Aidha ieneze utaalam huo kwa wazazi na jamii kwa njia ya semina, mafunzo, kwa njia ya vyombo vya habari n.k.

17.2.4. Utaalam wa ustawi wa jamii na wa kutunza na kulea watoto wasio wa kawaida uwe sehemu ya mafunzo katika vyuo vya ualimu.



Digitized by Google

17.2.5. Jamii isiwaone watoto wasio wa kawaida kama watu wasioweza lolote na wasiofaa kwa lolote. Mtazamo wa namna hii utawavunja moyo.

## 18.0. Mwisho

18.1. Utekelezaji wa Sera hii ya Malezi ya Taifa kwa ukamilifu utasaidia kuondoa au kupunguza matatizo yaliyoanza kujitokeza katika jamii na taifa letu.

18.2. Lakini mafanikio yake katika kuweka msingi ulio bora wa malezi na matunzo ya watoto na vijana wa taifa hili, utategemea mambo makuu yafuatayo:

18.2.1. Kila mzazi, kila mtanzania, kila taasisi, Wizara, Idara, Shirika, dhehebu na vikundi vya watu wanaohusika na malezi ya watoto, mahali popote, watekeleze wajibu wao ipasavyo kama ulivyofafanuliwa katika sera hii.

18.2.2. Utekelezaji kwa ukamilifu wa mipango, programu na sera nyingine mbalimbali za maendeleo ya jamii, siasa, uchumi na ustawi, kama vile:

(1) Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na Elimu ya Kujitegemea.

(2) Uimarishaji wa Elimu ya Msingi, Ufundi, Sekondari na Elimu ya Watu Wazima.

(3) Sera za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Uendelezaji wa teknolojia.

(4) Sera ya Chakula, Lishe, Afya n.k.

18.2.3. Usimamizi wa Chama katika kila ngazi utakaohakikisha kwamba kila anayehusika na utekelezaji wa sera hii ametimiza wajibu wake.



Digitized by Google

HQ 792
T34 C52
1987

HQ 792 .T34 C52 1987 C.1
Sera ya malezi ya taifaALJ6991
Hoover Institution Library
3 6105 082 324 539

Digitized by Google

Imepigwa Chapa na DUP,.
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Digitized by Google